epaper.ippmedia.com
www.ippmedia.com
0745 700710
LIKE & FOLLOW US
Jumatatu Oktoba 21, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MIAKA 30 Nipashe
Mwanga wa Jamii
www.ippmedia.com

# Nipashe

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0581836
www.ippmedia.com
nipasheTZ nipasheTZ The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital

UKURASA WA 5
**POMBE KALI ZAONGEZA WAGONJWA MOYO MIKOA YA KASKAZINI**



UKURASA WA 7
**WACHIMBAJI MADINI WADAIWA KUWANAJISI WATOTO ILI WAPATE MADINI MENGI**

UKURASA WA 17
**NMB YAPEWA TUZO BENKI YA KWANZA DUNIANI MFUMO WA 'LIPA KWA QR LINK'**



UKURASA 12
**WACHEZAJI MAJERUHI TANGU UKOSOAJI ONGEZEKO LA RATIBA**



Katibu Mwenezi Baraza la Wanawake Chadema (BAWACHA) Taifa, Aisha Machano.

## KIGOGO CHADEMA:

# Nilitekwa, nikateswa nimezindukia hospitalini

UKURASA 2



UKURASA WA 22
**TEN HAG AJIFUTUA KUIFUNGA BRENTFORD**

Wananchi wa wilaya ya Kyerwa wakimsikiliza Waziri wa Ujenzi, Innocent Bashungwa, wakati wa hafla ya kumkabidhi Mkandarasi Kampuni ya Shandong Luqiao Group eneo la mradi wa ujenzi wa barabara ya Kyerwa – Omurushaka (Km 50) kwa kiwango cha lami, mkoani Kagera mwishoni mwa wiki.



## Madaftari ya uandikishaji wapigakura yaibwa

UKURASA 5

## WAKOPESHAJI MTANDAONI

RIPOTI YA UCHUNGUZI

# Hawatambuliki BoT, BRELA; uendeshaji umejaa udhalilishaji

• **Riba** asilimia 80; raia wa kigeni washiriki kinyemela, Nipashe yabaini taasisi 21...*Endelea ukurasa wa 4*

**MICHEZO** GAMONDI ASIFU UBORA WA SIMBA UK.24 **KATUNI** UK.6

RIPOTI YA UCHUNGUZ

# Mchengerwa: Uandikishaji Uchaguzi Serikali za Mitaa umefanyika vizuri

Na Mwandishi Wetu

WAPIGAKURA 26,769,995 sawa na asilimia 81 ya lengo la kuandikisha wapigakura 32,987,579, wameandikishwa kwenye daftari la wapigakura wa Uchaguzi wa Serikali za Mitaa hadi kufikia juzi.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mohamed Mchengerwa, aliyasema hayo jana alipokuwa anatoa taarifa ya mwenendo wa uandikishaji wapigakura, kwa ajili ya uchaguzi huo kwenye Halmashauri ya Rufiji, mkoani Pwani.

Alisema hali ya uandikishaji wapigakuwa kwa siku tisa ni nzuri na jumla ya wapigakura 26,769,995 walikuwa wamejiandikisha kupiga kura sawa na asilimia 81.15 ya lengo la kuandikisha watu 32,987,579 kwa siku zote 10.

"Jumla ya uandikishaji kwa wanaume ni 13,033,988 sawa na asilimia 48.69 ya watu wote waliojiandikisha kwa tarehe 11-19 Oktoba, 2024 na wanawake ni 13,736,007 sawa na asilimia 51.31 ya watu wote waliojiandikisha," alisema.

Mchengerwa alitaja mikoa mitano yenye asilimia kubwa ya uandikishaji hadi kufikia tarehe 18 Oktoba, 2024 kuwa ni Tanga asilimia 101.13, ulifuatiwa na Pwani asilimia 98.74 kisha Mwanza asilimia 94.09, Dar es Salaama asilimia 86.66 na Dodoma asilimia 80.63 ya malengo.

Mchengerwa alisisitiza kuwa hakuna siku zitakazoongezwa kwa ajili ya uandikishaji wapigakura. Tarehe 20.10.2024, yaani jana saa 12:00 jioni ndiyo mwisho wa uandikishaji.



Waziri wa Ujenzi, Innocent Bashugwa, akizungumza na waandishi wa habari jana, mara baada ya kumaliza ziara yake kukagua ujenzi wa barabara ya mzunguko yenye urefu wa kilomita 112.3 inayotarajiwa kukamilika Machi, 2025. **PICHA PAUL MABEJA**

# Kigogo CHADEMA: Nilitekwa, nikateswa

Na Jenifer Gilla

KATIBU Mwenezi wa Baraza la Wanawake CHADEMA (BAWACHA) Taifa, Aisha Machano anayedaiwa kutekwa, kupigwa kisha kutupwa katika pori ameeleza namna tukio hilo lilivyofanyika hadi kujikuta akiwa Hospitali ya Rufani ya Mkoa Mwanayamala, Dar es Salaam.

Taarifa ya tukio hilo ilitolewa jana asubuhi na CHADEMA kupitia mitandao ya kijamii, chama hicho kikilihusisha na kitendo cha BAWACHA kuchoma vitenge vyenye picha ya Rais Samia Suluhu Hassan, wiki mbili zilizopita.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Aisha alisema kuwa juzi saa saba mchana, alipatwa na baa hilo akiwa wilayani Kibiti, mkoani Pwani, akitekeleza majukumu ya kichama ya kuhamasisha wananchi kujitokeza kugombea katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa.

Aisha alisema kuwa akiwa katika kituo cha daladala cha Bungu, alikutana na mwanamke ambaye alimchukulia kama abiria wa kawaida. Alipopanda katika basi na kukaa kiti cha mwisho, mwanamke huyo naye alipanda na kwenda kukaa karibu yake.

Wakiwa wanaendelea na safari, alilipa nauli na kumwelekeza utingo kuwa anashuka kituo kinachoitwa Jaribu na mwanamke huyo naye alilipa nauli na kuelekeza kuwa anashuka kituo hichohicho. Walipofika kituoni, mwanamke huyo alitangulia kushuka kisha naye akafuata nyuma yake.

Alidai kuwa wakati anavuka barabara kuelekea upande wa pili, kwa ajili ya kupanda bodaboda, lilikuja gari aina ya Landcruiser ambalo namba zake zinaanza na PT kisha wakashuka wanaume sita.

"Mmoja wao akaja akanigusa bega, akaniambia 'upo chini ya ulinzi, sisi ni polisi'. Nikamwambia 'ninaomba kitambulisho', akawa mkali. Wenzake wakaniambia 'ingia kwenye gari haraka, tunataka tuondoke, kuna mwanamke huyu hapa'.

"Wakati ninamwangalia yule mwanamke, nikagundua kuwa ni yule niliyepanda naye gari na kushuka naye," Aisha alisimulia.

Alidai kuwa alipoingia kwenye gari, yule mwanamke alimfunga pingu na mwingine (mwanamume) akimfunga kitambaa cheusi usoni kisha wakaanza safari ndefu saa 7:30 mchana na walifikia katika msitu ambao hakuutambua majira ya jioni.

Kwa mujibu wa Aisha, walipofika msituni, walimshusha na kumweka katika mti kisha wakaanza kumpiga kwa magongo sehemu mbalimbali za mwili, huku wakimwuliza ni nani aliyemtuma achome vitenge.

"Mimi nikawaambia kuwa sikutumwa, mimi ni kiongozi wa BAWACHA taifa, hivyo tuliandaa sisi viongozi na viongozi wetu wa mikoa tukafanya hilo tukio la kuchoma vitenge, na tulichoma kwa sababu kuna mambo yetu tulimwomba Rais Samia ayafanyie kazi, lakini hakuyafanyia kazi, ikiwamo vijana wetu watano waliopotea," alidai.

Alisema majibu hayo hayakuwaridhisha watu hao kwa kuwa waliendelea kumpiga na kumwambia kuwa kama asipowaeleza ukweli, wangemmaliza siku hiyo na kumlazimisha akiri kuwa walitumwa na viongozi wao wa chama.

Alitaja maelekezo mengine aliyodai walimpa ni kuwataja viongozi wa CHADEMA waliohudhuria mkutano na waandishi wa habari aliofanya hivi karibuni, Dar es Salaam na pia walimwuliza sababu za Katibu wa chama Mkoa wa Dodoma, kushiriki mkutano huo.

Baada ya kipigo cha muda mrefu, Aisha alidai walimfungua pingu na kitambaa kisha wakamvua nguo zote na kumpiga picha, wakamtishia kuwa akiitisha kikao na waandishi wa habari na kueleza yaliyotokea, watammaliza kabisa na kusambaza picha zake za utupu.

Alidai kuwa baadaye walimpandisha kwenye gari na kwenda kumshusha eneo lingine ambalo pia halifahamu kisha wakampa vitu vyake. Baada ya gari kuondoka, alinyanyuka na kufuata njia lilimopita gari hilo, huku akiwa anahisi maumivu makali na njaa.

Aisha alidai kuwa alitembea kwa muda mpaka akatokea eneo lenye kibanda cha kuuza chipsi na madereva wa bodaboda kisha akapoteza fahamu na alipozinduka, alijikuta yuko katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa Mwanyamala, Dar es Salaam na madaktari wakamweleza kuwa alipelekwa huko na bodaboda waliomwokota wilayani Kisarawe.

Alisema kuwa baada ya kuwaeleza madaktari, mkasa uliomkuta na kuwaonesha majeraha aliyonayo, aliandikiwa kuchukua vipimo vya X-ray ambavyo vilionesha kuwa hana majeraha yoyote makubwa ya ndani kama vile mfupa kuvunjika.

Aisha aliwaeleza BAWACHA kuwa wasikatishwe tamaa na tukio liliompata, bali waendelee kuhamasisha wanawake kujitokeza kugombea nafasi na kupigakura katika uchaguzi ujao.

**KAULI YA POLISI**

Jeshi la Polisi lilithibitisha kupokea taarifa ya kuokotwa kwa kiongozi huyo wa CHADEMA na limeanza uchunguzi kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu.

"Tunatoa wito kwa wananchi watulie, uchunguzi utatoa majibu sahihi ya nini kilichotokea dhidi yake, sababu zake ni zipi, wahusika ni nani na hatua zitachukuliwa kulingana na ushahidi utakaopatikana, kwa mujibu wa sheria," inasomeka sehemu ya taarifa ya Msemaji wa Jeshi Polisi nchini, DCP David Misime.


**KUPOTEA KWA CHETI**



**SALEHE HAMISI RAMADHANI** anatangaza kupotea kwa form four leaving certificate yenye index namba **S0870-0179** iliyotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **KILANGALANGA SECONDARY SCHOOL** mwaka 2019. Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **PHQ/PWA/KIB/21576/2024**

**KUPOTEA KWA KADI YA GARI**

**CHARLES DESIDERI HOTAY** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **NISSAN DUALIS** yenye namba **T 855 DWF.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo choccchote cha polisi. POLISI CONTROL NUMBER : **9910842747648.**

DANISH REFUGEE COUNCIL

**TANGAZO LA ZABUNI**

SHIRIKA LA KUHUDUMIA WAKIMBIZI LA DANISHI LINATARAJIA KUINGIA MKATABA WA HUDUMA ZA ULINZI WA OFISI NA MAENEO YA KAZI.

HIVYO SHIRIKA LA DANISHI LINATANGAZA ZABUNI TAJWA HAPO JUU NA WAZABUNI WAFUATE MAELEKEZO YAFUATAYO.

- USIFUTE KWENYE BEI
- USITUMIE WINO WA MAJI KUSAHIHISHA UNAPOFANYA KOSA.TUMIA KARATASI MPYA
- USIBADILISHE KARATASI ZA ZABUNI KWENDA KWENYE MFUMO WORD/EXCEL,
- ZINGATIA SEHEMU ZA KUSAINI NA KUGONGA MUHURI AMBAZO NI LAZIMA
- USISAHAU KUAMBATANISHA NYARAKA ZINAZOHITAJIKA KAMA VILE KIAMBATANISHO A.1, KIAMBATANISHO A.2, CHETI CHA KUKUBALI TUZO YA ZABUNI NA KANDARASI, WASIFU WA MUUZAJI NA FOMU YA USAJILI, HALI YA MKATABA WA JUMLA WA DRC, MAELEZO YA KAMPUNI, KANUNI YA MWENENDO WA WASAMBAZAJI WA DRC BAADA YA KUMALIZA SEHEMU ZOTE KAMILI, SAINI, GONGA MUHURI, WEKA TAREHE.

KWAHIYO SHIRIKA LA DANISHI LILILOPO KIBONDO LINAWAALIKA WAZABUNI KULETA BEI ZAO.

NYARAKA ZA KUJAZIA BEI ZINAPATIKANA KATIKA OFISI ZA DANISHI KIBONDO – MKOANI KIGOMA KUANZIA TAREHE 21.10.2024 HADI TAREHE 03.11.2024 SIKU ZA KAZI SAA 2:00 ASUBUHI MPAKA SAA 10:30 JIONI. TUNAPATIKANA BARABARA YA IRC KIBONDO KATIKA MKOA WA KIGOMA.

KWA MAWASILIANO ZAIDI PIGA +255621897518 au BARUA PEPE alan.mvano@drc.ngo

ZABUNI ZITAFUNGULIWA TAREHE 12.11.2024 SAA 4:00 ASUBUHI KATIKA OFISI ZA DANISHI KIBONDO KATIKA MKOA WA KIGOMA NA KAMATI YA KUFUNGUA ZABUNI.

UNAWEZA KURUDISHA ZABUNI KUPITIA RFQ.TZA@DRC.NGO AU KULETA MOJAKWA MOJA OFISINI KIBONDO – KIGOMA VINGINEVYO NI BATILI.

SIKU 100 OFISINI

# Kamishna Mkuu TRA akitaja mambo 10 ya kufanyiwa kazi

**Na Mwandishi Wetu**

KAMISHNA Mkuu wa Mamlaka ya Mapato (TRA), Yusuph Mwenda, ameelezea siku 100 za utumishi wake katika nafasi hiyo huku akisisitiza kuwa mamlaka hiyo inaamini katika kuwa na ushirikiano bora na uhusiano imara na walipakodi bila ya kuhatarisha ulipaji kodi stahiki kwa mujibu wa sheria.

Katika andiko lake la kushukuru, aliloliweka katika ukurasa wake wa mtandao wa Facebook, Kamishna Mwenda anasema anamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kibali cha kutimiza siku 100, akiwa Kamishna Mkuu wa TRA, baada ya kuaminiwa na kuapishwa na Rais Samia Suluhu Hassan.

"Ninamshukuru sana Mheshimiwa Rais, kuendelea kuniamini kumsaidia kusimamia uendeshaji wa TRA. Pia ninawashukuru viongozi wote wa serikali, wananchi na walipakodi wote, Mwenyekiti na Bodi ya Wakurugenzi ya TRA pamoja na watumishi wote wa TRA kwa ushirikiano mkubwa wanaonipa katika kipindi cha siku 100.

"Kwa pamoja tumethibitisha kwamba tunaweza kuwa na ushirikiano na uhusiano mzuri kati ya TRA na walipakodi, bila ya kuhatarisha ulipaji kodi stahiki kwa mujibu wa sheria kama tulivyofanya," anasema.

Anasema wanaweza kuongeza makusanyo ya kodi bila migogoro na walipakodi, kama ilivyowezekana katika makusanyo ya robo mwaka ya kwanza ya (Julai - Septemba 2024) kwa kuongeza asilimia 18 ya makusanyo ya kodi.

Mwenda ambaye kabla ya kuwa Kamishna Mkuu wa TRA, alikuwa Kamishna wa Mamlaka ya Kodi Zanzibar (ZRA), katika andiko lake hilo, anasema wanaweza kuwatembelea na kuwasikiliza walipakodi wa nchi nzima (kama walivyotembelea mikoa 25 nchi nzima, ili kuwasikiliza, kutatua migogoro yao ya kikodi kwa wakati pamoja na kuwa wabunifu wa kutumia mifumo rahisi ya kuwasikiliza, ili kupata mrejesho toka kwa wananchi na walipakodi wote.

"Tunaweza kuwekeza na kuharakisha ujenzi wa mifumo ya usimamizi wa kodi ya IDRAS na TANCIS ambayo inasomana na mifumo mingine, ili kurahisisha zaidi ulipaji na ongezeko la kodi, pia tunaweza kujenga mifumo ya kusimamia bandari zetu na mipaka yetu vizuri na kuweka mazingira ya ushindani yaliyo sawa, ili kuwezesha biashara na makusanyo ya kodi ya Forodha kuongezeka," anasema.

Kamishna Mwenda anasema wanaweza kuimarisha huduma za kodi pamoja na matumizi sahihi ya mfumo wa EFD na kuchukua hatua kwa wasiotumia kwa mujibu sheria za kodi, mifumo ya usimamizi wa kodi (EFDMS) na ushirikiswaji walipakodi.

Alitumia maadhimisho hayo ya siku 100 kazini kueleza kuwa wanaweza kuendelea kutoa elimu ya kodi kwa njia tofauti zenye tija na zinazoleta matokeo chanya, ikiwamo kuimarisha ukaguzi na uchunguzi, ili kuwatambua na kuwachukulia hatua wachache wanaokwepa kodi, kuleta usawa katika shughuli za kiuchumi nchini.

"Tunaweza kama TRA kuendelea kuongeza idadi ya walipakodi nchini, kuimarisha utoaji huduma nzuri, kuongeza weledi, ubunifu na uadilifu pamoja na kuwajali wateja wetu, ili kuimarisha ulipaji kodi wa hiari nchini," anasema.

Anasisitiza TRA itaendelea kushirikiana na wadau wote wa kodi, wakiwamo viongozi wa taasisi na jumuiya za wafanyabiashara nchini, ili kuendelea kujenga na kuimarisha mfumo wa kodi ulio sawa, unaotabirika, unaowezesha ukuaji wa biashara nchini, wenye ufanisi, utatuzi wa migogoro ya kikodi kwa haraka na unaohamasisha wananchi na wafanyabiashara kufurahia kulipa kodi kwa hiari.

Anatumia kaulimbiu ya 'Pamoja Tunajenga Taifa' kuwashukuru walipakodi wote na kuwahakikishia TRA itaendelea kutekeleza maagizo yote ya Rais ya kuwasikiliza walipakodi, kuendelea kutoa elimu ya kodi, kuweka mazingira wezeshi ya shughuli za kiuchumi nchini, kuimarisha utoaji huduma za kodi na kuendelea kufanya vizuri zaidi, ili kuiwezesha serikali kutimiza majukumu yake ya kuwaletea maendeleo wananchi.

# Bingwa wa nyonga, magoti Uingereza atua Mloganzila

**Na Joseph Mwendapole**

BINGWA wa Upasuaji wa Nyonga na Magoti kutoka Hospitali ya Queen Elizabeth ya Uingereza, Prof. Mamoun Abdel-Gadir, amewasili jijini Dar es Salaam, kwa ajili ya kambi ya matibabu ya siku tano kwa Watanzania.

Bingwa huyo kwa kushirikiana na wataalamu wa ndani, atafanya upasuaji huo kwenye kambi itakayofanyika katika Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH)-Mloganzila kuanzia leo.

Aliwasili jana katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere (JNIA), akipokewa na wafanyakazi wa Global Medicare, ambao wameratibu kambi hiyo kwa kushirikiana na MNH-Mloganzila.

Akizungumza wakati wa mapokezi hayo, Meneja Mkuu wa Global Medicare, Daniel Lazaro, alisema wamefurahi kuona amefika salama nchini na ujio wake utakuwa wa manufaa makubwa kwa watanzania wenye matatizo ya nyonga na magoti.

Prof. Gadir alishukuru serikali ya Tanzania na taasisi ya Global Medicare, kwa kuratibu vyema safari yake ya kuja nchini na aliahidi kutoa huduma bora kwa wagonjwa watakaojitokeza kwenye kambi hiyo.Mkurugenzi Msaidizi wa Huduma za Upasuaji wa MNH-Mloganzila, Dk. Goodlove Mfuko, alisema maandalizi yote yamekamilika na kwamba kwenye kambi hiyo watashirikiana na mtaalamu huyo.

"Mtaalamu huyu atashirikiana na madaktari bingwa ambao ni wataalamu wa mifupa na ajali Mloganzila, hii itakuwa mara ya pili kutoa huduma kama hii, kwani mara ya kwanza tuliwafanyia upasuaji wa kubadilisha nyonga na magoti wagonjwa 170 kwa mafanikio makubwa," alisema.

Aron Mwamyanda ambaye alifanyiwa upasuaji wa goti kwenye kambi iliyopita Mloganzila, alisema aliugua magoti kwa miaka mitatu na alizunguka hospitali nyingi bila mafanikio.


DTB DIAMOND TRUST BANK

**DTB na Lions Club Wafanikisha Kambi ya Macho Katika Hospitali ya Vijibweni, Kigamboni**

Diamond Trust Bank kwa kushirikiana na Lions Club Dar es Salaam, wamefanikisha kambi ya matibabu ya macho katika Hospitali ya Vijibweni, Kigamboni, ambapo wananchi walipata huduma ya matibabu ya macho bila malipo. Mpango huu ni sehemu ya dhamira ya DTB ya kuendelea kuchangia ustawi wa kijamii na kujenga afya bora. Katika kambi hii ya matibabu, zaidi ya watu 3,000 walipatiwa uchunguzi wa macho, na miwani 620 ilisambazwa kwa watu wenye uhitaji.

Tukio hili lilihudhuriwa na Mkurugenzi wa Kanda ya Afrika wa Shirika la Afya Duniani (WHO), ambaye pia ni Mbunge wa Jimbo la Kigamboni, Mh. Dkt. Faustine Ndugulile, ambaye aliipongeza juhudi za DTB za kuhakikisha kuwa huduma za afya zinawafikia wananchi, hasa katika sekta ya afya ya macho. Dkt. Ndugulile alisisitiza umuhimu wa miradi kama hii katika kuboresha afya ya jamii kwa ujumla na alitoa shukrani zake kwa ushirikiano endelevu kati ya DTB na watoa huduma za afya wa hapa nchini.

Mpango huu ni moja wapo ya hatua nyingi ambazo DTB inachukua ili kutimiza lengo lake la kuboresha upatikanaji wa huduma za afya, hasa kwa makundi yenye uhitaji zaidi. Kambi hii ya macho ni sehemu ya mkakati mpana wa uwajibikaji wa kijamii wa benki, unaolenga maeneo muhimu kama afya, elimu, na uendelevu wa mazingira.

"Tunaamini kuwa afya bora ni msingi wa maendeleo ya kijamii na kiuchumi. Ushirikiano wetu na Lions Club Dar es Salaam unaendana na maono yetu ya kuunga mkono maendeleo endelevu, kuhakikisha kila mtu anapata huduma za afya zenye ubora. Tuna dhamira ya kusaidia watu 10,000 kupata matibabu ya macho ifikapo mwaka 2030. Ni kazi kubwa lakini tumejipanga kuhakikisha kwamba tunatimiza lengo hili," alisema Bw. Ravneet Chowdhury (Mkurugenzi Mtendajo wa DTB) wakati wa kambi hiyo.

Kambi hii ya macho ni moja kati ya zile nyingi ambazo DTB imefadhili, ikiwa ni sehemu ya kujitolea kwake kuboresha maisha ya Watanzania. Mpango huu unakamilisha juhudi za benki katika kuleta athari chanya za muda mrefu kwa jamii za hapa nchini. DTB inaendelea kuendesha miradi kama hii ikiwa ni sehemu ya malengo yake ya uendelevu, ikiangazia afya, uhifadhi wa mazingira, na elimu.




*Mkurugenzi wa Kanda ya Afrika wa Shirika la Afya Duniani (WHO), ambaye pia ni Mbunge wa Jimbo la Kigamboni, Mh. Dkt. Faustine Ndugulile Pamoja na wafanyakazi kutoka benki ya Diamond Trust Bank Tanzania wakiwa katika ufunguzi wa kambi ya macho iliyofanyika hospitali ya vijibweni wilaya ya Kigamboni*



*Moja kati ya madakatari wakihudumia wagonjwa katika kambi ya macho iliyofadhiliwa na Diamond Trust Bank iliyofanyika katika hospitali ya Vijibweni wilaya ya Kigamboni*




*Mhe.Dr Faustine Ndugulile katika tukio la ugawaji miwani za macho kwa wahitaji zilitoloewa kwa ufadhili wa benki ya DTB uliofanyika kwenye hospitali ya Vijibweni wilayani Kigamboni*



*Wafanyakazi kutoka benki ya DTB Tanzania katika kambi ya macho iliyofanyika hospitali ya Vijibweni wilaya ya Kigamboni*

dtbtanzania

**Bank with us. Bank on us.**

**RIPOTI YA UCHUNGUZI**

## WAKOPESHAJI MTANDAONI

# Hawatambuliki BoT wala BRELA, uendeshaji umejaa udhalilishaji

**Na Mwandishi wetu**



SIKU 36 baada ya mwandishi wa gazeti hili kuwasilisha maswali Benki Kuu ya Tanzania (BoT), kutaka kujua kwanini wakopeshaji mitandaoni wanadhalilisha wakopaji, taasisi hiyo imetengeneza mwongozo kwa watoa huduma ndogo za fedha wa daraja la pili, wanaotoa huduma za mikopo kidijitali.

Agosti 19 mwaka huu, mwandishi wa habari hii aliwasilisha maswali BoT akitaka kujua, pamoja na mambo mengine, kama taasisi/kampuni zinazotoa mikopo mtandaoni zinatambuliwa na BoT na hatua inazochukua dhidi ya wakopeshaji wanaodhalilisha wakopaji.

Septemba 2, mwaka huu, BoT ilijibu maswali hayo, ikieleza kuwa haitambui taasisi hizo na kwamba imeshatoa tangazo kwa umma la katazo la kuendesha mikopo hiyo, mpaka watakapopata kibali cha BoT.

Katika majibu yake kwa mwandishi, BoT ilieleza kuwa Sheria ya Watoa Huduma Ndogo za Fedha, inaruhusu kutoa mikopo kwa njia ya mtandao, lakini mpaka wapewe kibali cha taasisi hiyo, ingawa hadi wakati huo hakuna hata mkopeshaji mmoja wa mtandaoni aliyekuwa amesajiliwa.

BoT pia ilithibitisha kumekuwa na malalamiko ya matumizi mabaya ya taarifa za waombaji mikopo ya mtandaoni.

Septemba 24, mwaka huu, ikiwa ni siku 36 tangu mwandishi wa Nipashe awasilishe maswali BoT, Naibu Gavana Dk. Yamungu Kayandabila, alitoa taarifa kwa umma kuwa wamechapisha Mwongozo wa Watoa Huduma za Fedha wa Daraja la Pili, wanaotoa huduma za mikopo kwa njia ya kidijitali.

Alisema kuwa mwongozo huo wa mwaka 2024 una lengo la kuimarisha usimamizi wa uendeshaji huduma za mikopo kidijitali.

"Mwongozo huu unalenga kuhakikisha uzingatiwaji kanuni za kumlinda mlaji wa huduma za kifedha, ikijumuisha uwazi, uwekaji bei, njia za ukusanyaji madeni, utunzaji taarifa za wateja na faragha.

"Kufuatia mwongozo huu, BoT inawaelekeza watoa huduma ndogo za fedha wa daraja la pili wanaotoa au wanaokusudia kutoa mikopo ya kidijitali, kutii matakwa ya mwongozo huu.

"Endapo mtoa huduma atakiuka agizo hili, BoT itachukua hatua za kiutawala, ikiwamo faini, kusitisha shughuli za utoaji mikopo ya kidijitali na kufutiwa leseni ya kuendelea na biashara ya huduma ndogo za fedha. BoT itachapisha orodha ya watoa huduma walioidhinishwa kutoa huduma kidijitali," alisema.

**UCHUNGUZI WA NIPASHE**

Uchunguzi uliofanywa na mwandishi wa Nipashe kwa miezi minne, umebaini utoaji mikopo mtandaoni kiholela. Ni mikopo yenye riba kubwa inayofika hadi asilimia 80, masharti ya mikopo yanafichwa, udhalilishaji wakopaji kwa kuundiwa makundi katika mitandao ya kijamii kisha picha zao kusambazwa, matumizi ya namba za simu zenye utambulisho (code) usiotambulika.

Mwandishi pia amebaini vijana wenye umri mdogo wamekuwa wanatumika kutukana na kudhalilisha wakopaji kwa njia ya simu, kutuma na kusambaza picha chafu zilizotengenezwa kwa lengo la kushinikiza mkopaji kulipa kiasi kisichostahili, wakopaji kupewa mkopo pungufu kinyume cha makubaliano ya awali na kuwapo raia wa kigeni wanaotumia teknolojia kutoa mikopo.

Katika uchunguzi wake, mwandishi pia amebaini wakopeshaji wana watumishi wanaodai kulipwa ujira kwa kadri wanavyokusanya, ofisi feki za wanaotoa mikopo na matangazo yenye udhamini katika mitandao ya kijamii ya Facebook na Instagram.

Vilevile, mwandishi amebaini kuwa mara baada ya mkopaji kutoa rukhsa ya taarifa zake binafsi kujulikana, wakopeshaji wanakuwa na uwezo wa kuingia katika akaunti yake ya Google na kuona mawasiliano yote kisha hutuma ujumbe ndani ya dakika moja, kwa watu wote walio katika orodha ya simu ya mkopaji kuwaarifa kuwa "huyu anadaiwa".

Uchunguzi pia umebaini wakopeshaji wanaingilia na kuendesha mawasiliano ya mtu, jambo ambalo limekuwa chanzo cha utapeli ukiwamo wa "zile fedha tuma katika namba hii".

Wakopeshaji hao wanakwenda mbali zaidi, kuna wakati wanavunja ndoa na baadhi ya watu kuripotiwa kujiua kutokana na madeni yasiyolipika; yanakuwa na riba inayoongezeka bila ufafanuzi rasmi.

Mwandishi alibaini hakuna mwongozo wala sheria ya kuwadhibiti hadi BoT ilivyotangaza mwongozo huo Septemba, mwaka huu. Ni hatua iliyopunguza kasi ya matangazo ya wakopeshaji hao katika mitandao ya kijamii, lakini baada ya wiki moja, matangazo hayo yalirejea kwa kasi.

Katika uchunguzi huo, ilibainika kuwa wakati wa kurejesha mkopo, namba inayopokea fedha imesajiliwa kama taasisi ndogo ya fedha. Mathalani, mkopaji aliyekopa kwenye App ya Bahari, aliporejesha, namba ilisoma ametuma kwa Stormtime Microfinace Company Limited.

**BRELA: HATUWATAMBUI**

Katika orodha ya 'applications' 21 za wakopeshaji ambazo mwandishi alifuatilia, hakuna iliyosajiliwa kwa jina tajwa (Stormtime Microfinace Company Limited) wala kutambuliwa na Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA).

Mwandishi aliingia katika mfumo rasmi wa BRELA wa kuangalia usajili wa kampuni na hakufanikiwa kupata kampuni yoyote yenye jina linalotumika mtandaoni kutoa mikopo.

Septemba 23, mwaka huu, Msajili wa Kampuni wa BRELA, Leticia Zavu, alisema walifanya mapatio katika Daftari la Msajili wa Kampuni na Daftari la Usajili wa Majina ya Biashara, lakini hawakuona majina yaliyoorodheshwa kwenye barua ya mwandishi wa gazeti hili aliyetaka kujua usajili wa Stormtime Microfinace Company Limited, App ya Bahari na nyinginezo ambazo mwandishi alikuwa anataka taarifa za usajili wake.

Katika barua yake kwa BRELA, mwandishi alikuwa na orodha ya majina ya wakopeshaji wafuatao wa mtandaoni: Mkopo wako; PesaX Tanzania; PataPesa-Instant Loans; OKOA MAISHA Finance, HiPesa-Mkopo Haraka Fast Loan; Fundflex; SwiftFunds; CashX: Online; BobaCash-Pesa&Usalama; GetLoan-Finance; Matupesa-Haraka Cash LoanFinance.

Wengine ni: Mkopo Huru; Branch: Quick Online Loan App; Flexi Cash-mkopo wa fedha; FinLoanOSafety, NoHiddenFees; TikCash, OnePesa; BahariPesa-Mikopo ya Mikopo Finance, Furaha Loan; na Zima Cash-instant Cash Loan.

Msajili Leticia alisema kuwa katika orodha hiyo iliyowasilishwa na mwandishi, walipata alama mbili za biashara ambazo ni Branch na Onepesa, na kwamba Branch inamilikiwa na Branch International Limited na imesajiliwa kwa kutoa huduma za fedha, bima na mali zisizohamishika (Real Estate), huku Bahari ikiwa na viashiria vya kuwa na uhusiano kibiashara na Stormtime Microfinance Company Limited.

Kwa mujibu wa msajili huyo, ufuatiliaji wao ulibaini Onepesa inamilikiwa na Mrisho Omari Sultani Trading as Baromo Micro-Credit na inatoa huduma za mikopo. Maombi ya usajili yameshapokewa na ilitangazwa siku 60 za mchakato wa usajili.

"Upekuzi umeonesha baadhi ya majina yanakaribiana na majina yaliyosajiliwa BRELA. Hivyo inawezekana wahusika wanajitambulisha kwa majina ambayo ni tofauti na yale ambayo yamesajiliwa na wanatumia majina kwa kufupisha.

"Kutokana na hali hii, tunashauri wateja kuhakikisha wanajiridhisha na uhalali wa usajili wa kampuni na majina ya biashara, kabla ya kuingia makubaliano yoyote ya kibiashara.

"Kutokana na watu wengi kujitambulisha kama kampuni zilizosajiliwa kutoa huduma za mikopo mitandaoni, tunapenda kuwakumbusha Watanzania kuwa huduma ya kupata uthibitisho wa usajili wa kampuni au jina la biashara, inapatikana kwa njia ya mtandao, yaani Online Registration System (ORS).

"Hivyo, wanatakiwa kutumia mfumo huo, ili kuzitambua kampuni halali zilizosajiliwa kutoa huduma kabla ya kufanya makubaliano yoyote," Msajili Leticia alisema.

Msajili Msaidizi wa BRELA, Seka Kasera, alisema ni lazima kuwe na msimamizi wa huduma ya mikopo inayotolewa, ili kuwa na usalama kwa wanaochukua na kutoa mikopo, baadhi ikiambatana na matangazo kwamba ndani ya dakika 15 mtu anapewa mkopo.

***ITAENDELEA KESHO**

## HABARI KITAIFA

# Madaftari ya Wakazi yaibwa, wanne washikiliwa na polisi

**Na Mary Mosha,** MOSHI

VITABU viwili vya kuandikisha orodha ya wapigakura katika Daftari la Makazi ambavyo tayari vilikuwa na orodha ya zaidi ya wapigakura 1,105, vimeibwa na katika kijiji cha Kikilelwa, wilaya ya Rombo, mkoani Kilimanjaro.

Kwa mujibu ya jana ya Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Nurdin Babu, watu wasiojulikana wameiba madaftari hayo katika kituo cha Josho, kilichoko kijiji cha Kikelelwa, kata ya Tarakea Motambu.

Vilevile, watu wasiojulikana wamevunja Ofisi ya Kijiji cha Kikelelwa (Kituo cha Lokoro) na kuteketeza kwa moto nyaraka mbalimbali, vikiwamo vitabu vya benki vilivyokuwa vikitumiwa na kijiji hicho.

Kijiji hicho cha Kikelelwa, kina wakazi 7,600 kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022.

Jana Mkuu wa Mkoa huo, Babu, alisema madaftari hayo yaliibwa na watu hao Oktoba 18 mwaka huu.

Tayari ameagiza vyombo vya dola, likiwamo Jeshi la Polisi, kuwasaka na kuwachukulia hatua wale wote waliohusika katika kuiba vitabu hivyo vyenye orodha ya wapigakura wa Uchaguzi wa Serikali za Mitaa uliopangwa kufanyika tarehe 27 ya mwezi ujao.

Alisema wilaya ya Rombo imetia dosari mkoa huo licha ya zoezi hilo katika wilaya nyingine kwenda vizuri.

"Wapo watu wenye nia ovu, wameamua kuiba madaftari yenye majina ya wananchi, lakini tumeshafanya juhudi ya kuwasiliana na TAMISEMI, kuomba kuongezwa muda wa kujiandikisha kwa wananchi wa Kikelelwa.

Kwa mujibu wa Babu, TAMISEMI imeridhia ombi hilo na kuongeza muda wa kujiandikisha wananchi wote walioorodheshwa katika kituo cha Josho, ambapo zoezi hilo litaanza upya na kutekelezwa mpaka Oktoba 28 mwaka huu.

Aliwataka wananchi wa eneo hilo kujitokeza kwa wingi, ili kuhakikisha wanapata haki ya kujiandikisha.

Jana, taarifa ya Jeshi la Polisi ilisema kuwa kwa kushirikiana na taasisi nyingine za kiuchunguzi, wanaendelea kuchunguza tukio la wizi wa madaftari mawili ya wakazi na kwamba watu wanne wanashikiliwa.

Pia wanachunguza jaribio la kuchoma moto Ofisi ya Mtendaji wa Kijiji cha Kikelelwa ambao unakwenda sambamba na kuwafuatilia waliopanga uhalifu huo.

"Jeshi la Polisi linafuatilia kwa karibu njama zilizopangwa na chama kimoja cha siasa za kuvamia na kupora vitabu vya kuandikisha wapigakura kwa madhumuni wanayoyajua wao wenyewe.

Tunatoa tahadhari kwa waliokaa na kupanga uhalifu huo kuwa ni kosa kisheria, wasithubutu kutekeleza njama hizo kwa kuwa hatua kali kwa mujibu wa sheria zitachukuliwa dhidi yao," alisema Msemaji wa Jeshi la Polisi, DCP David Misime.

"Jeshi la Polisi lingependa kuwahakikishia wananchi kuwa limejipanga vizuri kuhakiksha uandikishaji unakamilishwa vizuri na ambao hawajajiandikisha wasisite kujitokeza kujiandikisha bila hofu yoyote," aliongeza.

Mbunge wa Rombo, ambaye pia ni Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda, akizungumzia tukio hilo, alisema watu wasiojulikana walivamia ofisi ya kijiji na kurusha njiti ya kibiriti kwa dirishani na kuteketeza nyaraka mbalimbali.

"Katika kata hii hakuna shida yoyote, ni kikundi cha watu wachache kinachotaka kuleta doa katika zoezi hili, katika vituo vyote tumefika tunajiandikisha na mawakala wa vyama vyote wapo," alisema.

Baadhi ya wananchi katika eneo hilo, akiwamo Eunice Mmanda, walisema kilichofanyika ni "uhuni", serikali haipaswi kufumbia macho.

Unandikishaji wa wapigakura ulianza Oktoba 11 na ulikamilika jana. Wagombea wataanza kuchukua na kurejesha fomu Novemba 1-7 mwaka huu. Mikutano ya kampeni itaanza Novemba 20-26 mwaka huu.



Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Nurdin Babu.

# Pombe kali zaongeza wagonjwa moyo mikoa Kanda ya Kaskazini

**Na Tumaini Mafie,** ARUSHA

IDADI kubwa ya wagonjwa wa moyo wanaotoka mikoa ya Arusha, Kilimanjaro, Manyara na Tanga, wanapata maradhi hayo kutokana na unywaji wa pombe kali uliopitiliza, wataalamu wamebaini.

Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI), Dk. Peter Kisenge alisema mwishoni mwa wiki kuwa Kanda ya Kaskazini inaongoza kwa kuwa na wagonjwa wengi wa moyo nchini, akikitaja chanzo hicho kinachoongezwa msukumo na watu kutofanya mazoezi.

Dk. Kisenge alikuwa akitoa mrejesho kuhusu huduma za kibingwa zilizotolewa na serikali katika kambi ya siku tano ya matibabu jijini Arusha.

"Ndugu zangu, ugonjwa wa moyo husababishwa na unywaji wa pombe kali, lakini pia kutokufanya mazoezi, nayo ni sababu nyingine.

"Niwaombe wananchi hususani kanda hii ya kaskazini, mfanye mazoezi walau muwe na muda wa kutembea kama hakuna umbali wa kupanda gari au pikipiki.

Ni vyema ukatembea, inapunguza kwa kiasi kikubwa moyo kutanuka," alisema Dk. Kisenge.

Alieleza sababu ya kurudi Arusha kuweka kambi ya matibabu, ni kuendelea kuimarisha utalii, lakini pia kuvutia kufanya maandalizi ya kufungua Kituo cha JKCI Arusha, ili kujiandaa kwa michuano ya Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON) mwaka 2027.

Aliwataka wananchi kuwa na kawaida ya kupima afya zao, ili kubaini tatizo mapema na kulishughulikia, huku akieleza kuwa matibabu ya magonjwa ya moyo kwa hatua ya juu, hutumia gharama kubwa kuanzia Sh. milioni sita hadi 10.

Mkurugenzi wa Hospitali ya Arusha Lutheran Medical Center (ALMC), Dk. Godwin Kivuyo, alishukuru serikali kwa kuweka miongozo na sera za ubia kati ya taasisi za kidini na binafsi kuhakikisha suala la afya linakuwa na ahueni kwa wananchi kwa kupunguza gharama za matibabu.

"Ninashukuru serikali kwa kuweka miongozo na sera nzuri za ubia. Hili limetuwezesha kuingia makubaliano na JKCI kufanya kambi ya matibabu mwaka 2022 na mwaka huu, kwetu ni jambo la kushukuru," alisema.

Wakizungumzia kambi hiyo wagonjwa wanaoendelea kupatiwa huduma, wameeleza unafuu wanaopata katika huduma hiyo, huku wakisisitiza kuwa kufuata huduma hiyo jijini Dar es Salaam, uliwafanya wengi kushindwa kumudu gharama za usafiri na malazi.

Theresia Joel, mkazi wa Arusha, alisema kwao ni nafuu kusogezewa huduma hiyo karibu, akieleza kuwa kuifuata Dar es Salaam ni gharama mara mbili kutokana na gharama za nauli, malazi na chakula.

Akundaeli Kweka, mkazi wa Siha, mkoani Kilimanjaro, alisema kutokana na wagonjwa wengi kuwa na hali duni ya maisha, hulazimika kusalia nyumbani na kujitibu kwa kutumia dawa za kutuliza maumivu, huku wakishindwa kuhudhuria kliniki ya moyo.


## Afrisa Consulting Limited

T: +255 222773585
M: +255 75 886 8605
E: tza@afrisa.net
www.afrisa.net

* P.O. Box 66607
Dar-es-Salaam
TANZANIA

Plot 274, Block D
Bagamoyo Road, Kunduchi
Dar-es-Salaam
TANZANIA

**Cert of Incorp : 71729**
**TIN Reg No.: 108-443-650**
**VAT Reg No.: 40-004181-0**

Date: 15th October,2024

## VACANCY ANNOUNCEMENT

Afrisa Consulting Ltd is a registered entity in Tanzania which deals with Engineering Consulting services for the local authorities, provincial and national government, international organisations, and the private sector from blue chip to emerging entrepreneurs.
The company hereby invites applications from competent and experienced personnel to fill the vacancy whose detailed information appears herein: -

**1.0 OCCUPATIONAL HEALTH AND SAFETY OFFICER - 1 POST**

**1.1 Duties and Responsibilities**
- Risk assessment,
- OHS audit and inspections,
- Emergency and incident response and reporting,
- Incident investigation.

**1.2 Qualifications and Experience**
- Must be a holder of bachelor's degree or Diploma in occupational health and safety.
- Certificate from National Examination Board in Occupation Safety and Health (NEBOSH) will be an added advantage.
- Minimum of eight (8) years post-qualification working experience in road work construction activities.
- A minimum of four (4) years of full-time relevant operational experience on risk assessment, OHS audit and inspections, emergency and incident response and reporting, incident investigation, and OHS management systems during road construction in developing countries.
- Should have strong knowledge and experience in supervision of implementation of OHS management systems in road construction with at least two road projects funded by the Multilateral Financing agencies in the last three (3) years.
- Must be able to speak both English and Swahili languages.

**1.3 Remuneration**
According to Company Pay Scale.

**2.0 Mode of application**
All applications should be sent via **lightness@afrisa.net** copy to **saula@afrisa.net**
**Phone No.+255222773585**
**Deadline is on Monday 25th October ,2024.**

**Only shortlisted applicants will be contacted.**

# MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## TFF, TPLB imetosha, sasa leteni waamuzi wa 'dabi' kutoka nje

**MECHI** ya watani wa jadi, Simba na Yanga imemalizika kwa lawama kutoka kwa mwamuzi, Ramadhani Kayoko, ambaye mbali na wadau wengi wa soka, lakini pia wanachama na mashabiki wa 'Wekundu wa Msimbazi' wanamtuhumu kuwanyima penalti mbili za wazi.

Hii si mara ya kwanza kwa mashabiki wa soka kulalamika juu ya udhaifu wa makusudi au wa bahati mbaya kwenye michezo ya dabi. Kwa miaka ya hivi karibuni waamuzi wa Tanzania wanaonekana kushindwa kabisa kumudu kucheza michezo hii inayozihusu timu hizi.

Wamekuwa wanasita au kuogopa kutoa maamuzi magumu licha ya kwamba makosa yanaonekana wazi. Kwa mfano kwa mechi ya juzi kwa marudio ya televisheni, haikuhitaji wala VAR kujua Kibu Denis alikuwa amechezewa madhambi ndani ya eneo la hatari na wachezaji wa Yanga mara mbili na mwamuzi akapuuzia.

Kwa mtazamo na maoni ya wadau wengi wa soka, wanasema hata adhabu ambayo mwamuzi huyo aliikubali ni kwa sababu tu ilikuwa nje ya boksi na haikupaswa kuwa penalti.

Tumeona mashabiki wa Simba wakilalamika sana na wengine wakiapa kuwa hawatoenda tena uwanjani wala kuangalia mipira vibandani.

Wanadai kuwa kwa mechi za hivi karibuni wamekuwa wakinyimwa haki yao ya kupata penalti, wakikumbushia mchezo uliopita wa Agosti 8, mwaka huu kwenye nusu fainali ya Ngao ya Jamii.

Alikuwa ni Kijili ambaye aliangushwa na Boka, ndani ya boksi ambapo ingeweza kuwapa nafasi ya Simba kusawazisha, lakini mwamuzi Ahmed Arajiga hakutoa adhabu hiyo.

Na juzi imejitokeza hivyo hivyo na wanaamini wamenyimwa, hivyo wanaona kama wao hawana haki ya kutendewa ndani ya dakika 90 kwenye michezo ya dabi.

Tunavyoona, kwa uchezeshaji huu wa waamuzi tutaendelea kupoteza watazamaji wengi uwanja na hata kwenye vibanda umiza na kumbi za starehe ambako hukusanyika kufuatilia mechi hizo.

Siku zote mashabiki wa soka hukubali wanapofungwa, lakini wanapoona wanapoteza kwa namna ambayo wanaonewa huona hakuna maana yoyote ya kuendelea kuweka akili, nguvu na pesa kwa kitu ambacho wanaona haki haitendeki.

Kwa hili tunawaomba Bodi ya Ligi ya TFF (TPLB), iangalie suala hili kwa makini, ikiwezekana waamuzi wa mchezo huu wawe wanatoka nje ya nchi kama ambavyo nchi nyingi za Afrika sasa hivi zinafanya.

Dabi zote kubwa za Afrika kwa sasa waamuzi huwa wanatoka nje ya nchi, kuanzia Misri, Morocco, Tunisia, Algeria hata Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo na Afrika Kusini.

Kama dabi ya Tanzania ni ya sita Afrika kwa ubora, iweje iendelee kutiwa aibu na doa kupitia waamuzi hawa ambao wanaonekana kushindwa kuimudu? Tunatambua kwa wenzetu waliamua hayo, baada ya kutokea fujo viwanjani na machafuko ambayo mengi yamesababishwa na waamuzi.


Hatutaki kufika huko, hivyo ni vizuri zaidi kuzuia kuliko kutibu, fikiria kwamba mchezo unaofuata, halafu itokee mwamuzi tena awanyime penalti kama hivi huwezi kujua nini kitatokea.

Tunachowashauri TPLB, sasa imetosha, ifanye iwezekanavyo kuwaleta waamuzi kutoka nje ya nchi, hata nchi za jirani tu, kama Burundi, Kenya, Rwanda, Sudan, Somalia, Eritrea ambako kuna waamuzi bora tu na wengi huchezesha fainali za AFCON na michuano ya Ligi ya Mabingwa na Kombe la Shirikisho Afrika.

Na ikiwezekana wasiwe hata wanatangazwa, kwani si lazima kufanya hivyo. Kama listi ya wachezaji inatolewa dakika chache kabla ya mchezo kuna haja gani ya waamuzi itoke wiki, au siku tatu kabla ya mchezo?

Hilo likifanyika, tunaamini litapunguza kwa kiasi kikubwa kelele hizi ambazo zinawahusisha waamuzi kuwa vinasaba (DNA) na moja kati ya timu hizo wapopewa dhamana ya kuzichezesha.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji:** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com




# Muungwana Lazima Nilonge



## Waamuzi msitake kuitoa 'dabi' ya utani kwenda kuwa ya uadui

Na Adam Fungamwango

**TOKA** juzi huwezi kuwaambia baadhi ya mashabiki wa Simba kuwa dabi dhidi ya Yanga ni utani wa jadi akakuelewa.

Ni kwa sababu wanaona hawakufungwa kihalali. Walipaswa kama si kushinda basi angalau watoke sare kutokana na kunyimwa penalti mbili ambazo wao wanadai ni halali. Marudio ya picha za televisheni yanaonesha hivyo.

Ramadhani Kayoko hakuona, hakuwa makini au alipotezea na kusababisha mashabiki wa Simba kucharuka hasa baada ya kufungwa bao dakika za jioni.

Kumbukumbu zinanipeleka katika mchezo uliopita ambako pia mashabiki wa Simba walilalamika kunyimwa penalti ambayo ingeweza kuwapa sare kwenye mchezo wao dhidi ya Yanga na kuwapeleka kwenye mikwaju ya penalti katika mchezo wa nusu fainali ya Ngao ya Jamii.

Kwa sasa mashabiki wa Simba wanachoamini ni kwamba kumekuwa na uonevu kwa timu yao kwani matukio mengi ya makosa ya waamuzi yamekuwa yakiangukia kwao.

Mioyoni wameanza kuitoa mechi yao na Yanga kama utani wa jadi na kutaka kuiweka kwenye uadui kwani wanaona pamoja na jitihada wanazozifanya, lakini wanaangushwa na maamuzi ya waamuzi.

Ikumbukwe mechi za Simba na Yanga zilianza rasmi kuchezwa 1937, baada ya timu zote mbili kuwa tayari zimeanzishwa.

Yanga ilianzishwa rasmi Februari 11, 1935 na Simba ilianzishwa 1936, na zilikuwa zikicheza michezo kwenye vikombe mbalimbali jijini Dar es Salaam, kabla ya kuanzishwa rasmi kwa Ligi Kuu, iliyotambulika wakati huo kama Ligi ya Taifa mwaka 1965, wakati huo bado ikiitwa Sunderland.

Kwa miaka hiyo yote mechi za dabi zimekuwa za kitamaduni zaidi na ni tofauti na dabi zingine katika nchi zingine ambazo zimekuwa na uhasama kiasi cha watu kuuana.

Hapa nchini ni mechi za utani wa jadi na unaweza kuona mashabiki wa Yanga wakishinda wanaweza kuwanunulia chakula na vinywaji wenzao wa Simba huku wakiwazodoa, kitu ambacho unaweza usikikute nchi zingine.

Utani huu ndiyo umeweza kuifanya dabi hii kuwa bora na maarufu zaidi na kuua zile za Gor Mahia na AFC Leopards ya Kenya na hata SC Villa na Experess za Uganda.

Dabi ya Tanzania ndiyo ya ajabu zaidi kwani familia moja inaweza kugawanyika wengine wakawa Simba na wengine Yanga, tofauti na baadhi ya nchi ambazo familia yote na hata majirani wanakuwa ni timu moja kwa sababu wanashangilia timu inayotoka ukanda huo tu.

Yaani kama timu inaitwa Kinondoni FC, basi watu wote wa huko wanakuwa mashabiki wa timu hiyo, hivyo familia nzima na wanaowazunguka wote mnakuwa timu moja.

Pamoja na yote hayo, watu wameendelea kuwa wamoja kutokana na uadilifu mkubwa wa waamuzi katika michezo ambayo wanakutana.

Hata Yanga walipofungwa mabao 6-0 mwaka 1977 hakukuwa na tuhuma za mwamuzi, 5-0 mwaka 2012, hata Simba walipofungwa mabao 5-1 msimu uliopita, hakuna shabiki yoyote aliyelia na refa zaidi ya kudai wachezaji wao wameshachoka na hilo liliwafanya kuondoa wengi.

Kwa maana hiyo kilio cha wanachama na mashabiki wa Simba kisipuuzwe, kwani uchezeshaji huu unaweza kuwafanya waone Yanga ni maadui zao na si watani wa jadi tena.

Hili litafutika kwa Shirikisho la Mpira wa Miguu (TFF), na Bodi ya Ligi kukaa chini na kusaka mustakabali wa hili, dabi ichezeshwe kwa haki na ionekane kuwa imetendeka, ili aliyefungwa ampe mwenzake mkono, vinginevyo kunaweza kuzuka matatizo mbele ya safari.

Imetosha kuona mechi za dabi za siku za karibuni waamuzi ndiyo 'wanaotrendi' zaidi na kuzungumzwa na mashabiki na wachambuzi kuliko uwezo wa wachezaji wanaouonesha uwanjani.

Kwa haya wanayofanya waamuzi wanafanya hata mashabiki kupendekeza sasa hata mwamuzi awe na nafasi ya kuchaguliwa katika Tuzo ya Mchezaji Bora wa Mechi ('Man of The Match'), kutokana tu na tabia yao ya kuzifinyanga sheria 17 za soka kwa kuamua matokeo.

TFF na Bodi ya Ligi, wanapaswa kuilinda tunu ya dabi ya Kariakoo iendelee kuwa ya utani wa jadi badala ya uadui kwa kuhakikisha mpira unachezeshwa kwa haki bila kumpendelea yoyote yule.

Mashabiki wengi wa soka duniani huwa wanaridhika wanapofungwa kihalali, lakini si kwa utata kama mechi hii.

# Afanyiwa upasuaji wa moyo kwa Zoom

**Na Christina Mwakangale**

MGONJWA ambaye mishipa ya moyo ya damu iliziba, amefanyiwa upasuaji wa tundu dogo kwa njia ya mtandao (Zoom), chini ya wataalamu wa Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI) na wenzao kutoka nchi mbalimbali duniani.

Bingwa wa Magonjwa ya Moyo wa JKCI, Dk. Khuzeima Khahbhai, alisema mwishoni mwa wiki kuwa wamefanikiwa kubadilisha valvu za moyo na kuzibua mishipa kwa kushirikiana na wataalamu kutoka sehemu mbalimbali kwa njia ya mtandao.

Dk. Khuzeima alisema jijini Dar es Salaam kuwa kwa kutumia teknolojia hiyo, mgonjwa anakuwa hana majeraha makubwa na baada ya siku mbili anaruhusiwa kurudi nyumbani tofauti na kama upasuaji ungekuwa wa kufungua kifua.

"Tumefanya upasuaji wa kubadilisha valvu za moyo na kuzibua mishipa ya damu bila kufungua kifua. Mgonjwa yupo salama na sasa tunategemea baada ya siku mbili ataruhusiwa kwenda nyumbani.

"Upasuaji huu unaitwa TAVI, tulikuwa tukiufanya mbashara kupilia mkutano wa Zoom kwa kujumuika na madaktari wenzetu kutoka sehemu mbalimbali duniani, kwa lengo la kubadilishana ujuzi na kujifunza jinsi upasuaji huu unavyofanyika," alisema Dk. Khuzeima.

Bingwa wa Magonjwa ya Moyo kutoka India, Dk. Meghav Shah, alisema ni mara yake ya kwanza kufika Tanzania, akisema uwekezaji wa vifaa vya kisasa katika taasisi hiyo umeongeza uwezo mkubwa katika huduma.

"Nimeshangazwa na vifaa vya kisasa vilivyopo hapa (JKCI), mitambo yao ni ya kisasa, inaonesha picha nzuri sana ninaona taasisi hii ikikua zaidi na zaidi itakuwa kitovu kikubwa cha matibabu ya moyo Afrika," alisema Dk. Meghav.

Mgonjwa aliyefanyiwa upasuaji huo, Thomas Sagawe, alisema alikuja JKCI baada ya kupata rufani kutoka Kilimanjaro Christian Medical Centre (KCMC), ambako alifanyiwa vipimo. "Nilipimwa na kugundulika kuwa na shida kwenye moyo, nilipewa rufani ya kufika JKCI, nilipokewa vizuri na kufanyiwa vipimo tena, ninaona sasa ninaendelea vizuri, ninawashukuru sana kwani huduma zao ni nzuri sana," alisema Sagawe.

Mwanawe, Paul Thomas alisema kufanyika kwa upasuaji huo ndani ya nchi kumewasaidia kuokoa gharama za fedha na muda ambao wangetumia kama wangeenda kumtibu mzazi wake nje ya nchi.

"Kuwapo huduma hii nchini kumetusaidia, hatujatumia fedha nyingi kulinganisha na ambazo tungetumia kama tungeenda kutibiwa nje ya nchi.

"Nitumie nafasi hii kuwaambia Watanzania wenzangu, wakihitaji huduma za matibabu ya moyo wasihangaike kwenda nje, huduma zipo hapahapa nchini," alisema Paul.



Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu), Ummy Nderiananga, akifafanua jambo wakati wa semina ya kuijengea uwezo Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria kuhusu Baraza la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (NEEC), iliyoandaliwa na baraza hilo, mwishoni mwa wiki ukumbi wa Bunge, jijini Dodoma. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wachimbaji madini wadaiwa kuwanajisi watoto wakiamini watapata madini mengi

**Na Thobias Mwanakatwe,** SONGWE

MKUU wa Wilaya ya Songwe mkoani Songwe, Solomon Itunda, amewataka wachimbaji madini kuondokana na imani potofu kwamba wakibaka au kulawiti mtoto ndogo, watapata madini mengi.

Alisema hayo juzi wakati akizungumza na wachimbaji madini katika kata ya Saza wakati wa maonesho ya dhahabu yaliyofanyika katika kata hiyo na kuwashirikisha wachimbaji wadogo na wakubwa wa dhahabu.

"Katika maeneo yetu haya ya uchimbaji, kuna watu wana imani za kishirikina kwamba eti akimnajisi au kumlawiti mtoto mdogo, atapata dhahabu, watu hao tutawakamata wote wanatuharibia watoto wetu," alisema.

Itunda alipongeza Jeshi la Polisi kwa kuwa limekuwa linachukua hatua kwa wanaofanya matukio hayo; wapo walifikishwa mahakamani na kufungwa jela miaka 30 au kifungo cha maisha.

"Dawa yao ipo motoni, wale ambao wana mawazo yaliyolala, eti ukimbaka au kumlawiti mtoto utapata dhahabu nyingi, serikali iko makini, hawatabaki salama, watachukuliwa hatua," alionya.

Mkuu wa Wilaya pia alipiga marufuku wachimbaji kuwatumia watoto katika machimbo, wakibainika watachukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria.

"Kupitia hadhara hii, ni marufuku kuendelea kuwaajiri watoto katika machimbo, jukumu la watoto ni kwenda shuleni kusoma. Yeyote atakayebainika amewaajiri watoto wadogo, hatua kali zitachukuliwa dhidi yake," alionya.

Aliwataka wachimbaji kuzingatia sheria za nchi kwa kuhakikisha wanakuwa na leseni wanapotekeleza shughuli zao za uchimbaji.

Kuhusu usalama, Mkuu wa Wilaya aliwataka wachimbaji kuuimarisha katika machimbo kwa kuweka 'matimba' (uzio maalumu unaojengwa kuzuia mmomonyoko katika mgodi wa dhahabu), ili kuzuia mvua inaponyesha maji yasiingie ndani ya shimo.

**KABWELA** — Na Fadhili Mohammed



# Kisarawe kuchangisha fedha ujenzi jengo la VIP

**Na Julieth Mkireri,**
KISARAWE

MKUU wa Wilaya ya Kisarawe, Petro Magoti na Mbunge wa Kisarawe, Dk. Selemani Jafo wanatarajiwa kuongoza hafla ya uchangiaji fedha za ujenzi wa jengo maalumu la kulaza wagonjwa (VIP).

Ujenzi wa jengo hilo katika Hospitali ya Wilaya ya Kisarawe, unafanywa kutokana na uhitaji uliopo kwa sasa kulinganisha na mwaka 1990 lilipojengwa jengo la awali ambalo halikidhi mahitaji ya sasa.

Hafla hiyo ambayo imeandaliwa na wadau wa afya kwa kushirikiana na madaktari wa hospitali hiyo, inatarajiwa kufanyika mwanzoni mwa mwezi ujao na kuwashirikisha wadau mbalimbali ndani na nje ya mkoa wa Pwani.

Akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake mwishoni mwa wiki, Magoti alisema fedha zitakapopatikana katika hafla hiyo, zitatumika kujenga jengo hilo pamoja na kukarabati majengo mengine ambayo yameanza kuchakaa.

Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Wilaya ya Kisarawe, Dk. Yona Kabata, alisema jengo maalumu lililopo kwa sasa, lina uwezo wa kulaza wagonjwa tisa pekee. Lilijengwa mwaka 1990, yaani miaka 34 iliyopita.

Dk. Kabata alisema fedha hizo zitakapopatikana zitatumika kujenga jengo hilo maalumu linalotarajiwa kuwa na vyumba 30 hadi 50 na litasaidia kutatua changamoto iliyopo ya uhaba wa miundombinu unaokwamisha baadhi ya wagonjwa kulazwa katika hospitali hiyo.

"Wapo wagonjwa mpaka wa nje ya nchi wanafika hapa kutaka kulazwa VIP, lakini hatuna jengo linaloendana na hali ya sasa, pia nafasi inakuwa haitoshi, hivyo tunawaomba wadau wajitokeze kutuchangia tupate jengo jipya pamoja na kukarabati majengo mengine," alisema.

Baadhi ya wagonjwa waliozungumza na waandishi kuhusu jengo la sasa, waliomba jengo hilo liboreshwe, ili liendane na wakati wa sasa na kuwa na uwezo wa kuchukua wagonjwa wengi.

# Maboresho NIDA yaondoa usumbufu

**Na Kulwa Mzee**

MABORESHO yaliyofanywa katika kituo cha huduma ya wateja cha Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA), yataongeza ufanisi na kuondoa usumbufu wa kupata huduma, wadau wamesema.

Wadau hao wametoa maoni hayo siku chache baada ya mamlaka hiyo kutangaza kufanyia maboresho makubwa kituo chake cha huduma kwa wateja

(Call Centre) na kueleza kuwa, kitakidhi matarajio ya Watanzania wengi.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti, wadau hao akiwamo Yassin Chuma ambaye ni mjasiriamali kutoka Mabibo Sokoni, alisema maboresho yaliyofanywa yatatoa wigo kwa wananchi wengi kujua taarifa zao binafsi zinazofanyiwa kazi na mamlaka hiyo.

Alisema kwa wafanyabiashara, wakiwamo wajasiriamali wadogo, maboresho hayo yamekuja wakati mwafaka kwa sababu ya uhitaji mkubwa wa namba ya NIDA, kwa ajili ya matumizi mbalimbali.

"Maboresho yamefanyika wakati sahihi ambao watu wengi hawana namba wala vitambulisho vya NIDA, hivyo kuwapo namba hii kutasaidia hata wale ambao hawajajiandikisha, watatumia kwa kupiga simu kwa watoa huduma na kuhudumiwa bila kwenda ofisi za mamlaka hiyo," alisema Chuma

Anna Msuya, mkazi wa Kigamboni, mkoani Dar es Salaam, alisema maboresho hayo yatapunguza urasimu uliokuwapo awali kupata namba au vitambulisho kutokana na maofisa au mawakala wachache waliokuwa siyo waaminifu.

"Siku hizi mambo yanakwenda kidijiti, maboresho haya ni muhimu na hivyo yataleta mageuzi makubwa ndani na nje ya NIDA, pia kuongeza imani kwa chombo hicho," alisema Anna.

Atupele Mwakalinga, mwanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), alisema maboresho hayo yatasaidia wanafunzi, hasa wale wanaotarajia kujiunga na vyuo vikuu kwa ajili ya kupata mikopo kutoka Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB), kwa kuwa moja ya vigezo vya kupata mkopo ni kuwa na namba ya NIDA.

"Wanafunzi wengi wanashindwa kupata mikopo ya elimu ya juu kutokana na kutokuwa na namba wala kitambulisho cha NIDA, ujio wa namba hii ya huduma kwa wateja utasaidia wanafunzi wengi kupata namba au kitambulisho cha NIDA na kupata mikopo," alisema Mwakalinga.

Akizungumza na waandishi wa habari hivi karibuni jijini Dar es Salaam, Ofisa Habari Mkuu wa NIDA, Geofrey Tengeneza alisema kuwa mpaka sasa wamezindua mfumo wa usajili kupitia mtandao, ambao mwananchi anaweza kuanza hatua za mwanzo za usajili kupitia tovuti yao na kumwezesha kufuatilia na kufahamu maombi yake yalipofikia.

Alisema maboresho hayo ni pamoja na mabadiliko ya namba za simu ambapo kuanzia Oktoba 28 mwaka huu, namba itakayokuwa inatumika ni 0232210500 ya TTCL na namba nyingine za mitandao mbalimbali zilizokuwa zinatumika awali hazitatumika tena baada ya tarehe hiyo.

Mbali na uzinduzi huo wa namba maalumu itakayotumika kuwasiliana na wateja wake, NIDA pia imejipanga kuongeza idadi ya watoa huduma katika kituo hicho cha huduma kwa wateja, ili kurahisisha mawasiliano na wateja.

"Kuna baadhi ya changamoto zitatatuliwa wakati huohuo na watoa huduma wetu, mwananchi anapopiga simu na mengine yatapokewa na kujibiwa kulingana na shida ya mtu.

"NIDA inalenga kila simu ya mteja inayopigwa iweze kupokewa, ndio maana tumepanga kuongeza idadi nzuri ya watoa huduma kwa wateja, ili kila simu ipokewe," alisema.



Mbunge wa Jimbo la Kavuu na Naibu Waziri wa Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Geophrey Pinda (wa tatu kushoto waliosimama), akiwa katika mstari wakati wa kujiandikisha kwenye orodha ya wapigakura, kwa ajili ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa katika mtaa wa Ndemanilwa, Kata ya Kibaoni, halmashauri ya Mpimbwe, mkoa wa Katavi. **PICHA: MUNIR SHEMWETA**

# Laini za simu zaongezeka hadi milioni 80 nchini

**Na Salome Kitomari**

RIPOTI ya takwimu za mawasiliano kwa robo ya mwaka inayoishia Septemba 2024 iliyotolewa na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), inaonesha idadi ya laini za mtu kwa mtu zilizosajiliwa imeongezeka kutoka milioni 76.6 hadi milioni 80.7 ikiwa ni ongezeko la asilimia tano katika kipindi hicho cha miezi mitatu.

Ripoti hiyo ambayo ilitolewa juzi na TCRA, inaonesha laini za simu za mkononi na mezani, kwa kampuni tano za simu zimeongezeka kutoka milioni 75.6 hadi milioni 79.6 sawa na ongezeko la asilimaa 5.4 katika kipindi hicho.

Vilevile, laini za mashine kwa mashine kwa kila mtoa huduma zimeongezeka kutoka 995,494 hadi milioni 1.02 ikiwa ni ongezeko la asilimia 4.8.

Ripoti hiyo inabainisha kuwa Dar es Salaam ilishika nafasi ya kwanza kwa kuwa na laini milioni 14.8, ikifuatiwa na Mwanza yenye laini milioni 5.3, Arusha milioni 4.9, Mbeya milioni 4.6 na Dodoma milioni 4.3.

Kwa upande wa Zanzibar, mikoa yenye laini chache zilizosajiliwa katika robo ya kwanza ni Kaskazini Unguja yenye laini 73,743, Kusini Unguja yenye laini 110,970, na Kusini Pemba yikiwa na laini 124,472.

Ripoti inaonesha kuwa wakati bei za kupiga simu ndani na nje ya mtandao, SMS kitaifa (local SMS), SMS kimataifa na data hazikubadilika, bei za kupiga simu za Afrika Mashariki zilipungua kwa asilimia mbili na mataifa mengine ziliongezeka kwa asilimia nne. Ripoti hiyo pia ilionesha kuwa watoa huduma wote hutoza Sh. 30 kwa dakika ndani na nje ya mtandao, isipokuwa Halotel inayotoza Sh. 10 kwa dakika ndani ya mtandao na Sh. 20 nje ya mtandao.

"Wastani wa bei ya huduma ya sauti ndani ya mtandao katika robo ya mwaka inayoishia Septemba 2024 ilibaki sawa na robo ya mwaka inayoishia Juni 2024.

"Bei ya huduma ya sauti kimataifa zilitofautiana baina ya watoa huduma. Wastani wa bei ya huduma ya sauti kwa dakika moja kwa Afrika Mashariki na nchi nyingine ni Sh. 696.68 na 1,948.22, mtawalia," inabainishwa katika ripoti hiyo.

Kuhusu idadi ya dakika za huduma ya sauti ndani na nje ya mtandao nchini kwa robo ya mwaka inayoishia Juni 2024 na Septemba 2024, ripoti inaonesha kuwa Julai 2024 ulikuwa mwezi wenye dakika nyingi zaidi kulinganishwa na miezi mingine ya robo ya mwaka huo.

"Takriban dakika bilioni 41.1 zilitumika katika robo mwaka iliyoishia Septemba 2024 kulinganishwa na dakika bilioni 39.6 katika robo mwaka iliyoishia Juni 2024. Hata hivyo, idadi ya dakika ndani ya mtandao ilikuwa kubwa zaidi kulinganishwa na nje ya mtandao katika robo ya mwaka iliyoishia Juni 2024," inaelezwa katika ripoti hiyo.



Mkuu wa Mkoa wa Manyara, Queen Sendiga (kulia) akigawa nyama pori alipofika jana bonde la Yaeda Chini, kijiji cha Mongowamono wilayani Mbulu, kuhamasisha wawindaji, waokota matunda na warina asali wa jamii ya Wahadzabe washiriki kujiandikisha kwenye daftari la makazi ili waweze kupiga kura ya kuwachagua viongozi wa Serikali za mitaa. **PICHA: GIFT THADEY**

# Utafiti wabaini ongezeko vijana wa kiume kulawitiwa

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

UTAFITI uliofanywa kwa siku tisa na Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP) na wanajamii wanaotoka vijiji vinane vya kata ya Mabogini, wilayani Moshi, mkoani Kilimanjaro, umebaini ongezeko la ukatili wa kingono, hasa ulawiti kwa vijana wa kiume katika eneo hilo.

Maeneo ya Kwa Manosa na Bogini Juu yametajwa ndiko ukatili huo unaendelea, vijana wa kiume wakilawiti kwa kundi, ambapo ndani ya wiki moja mwezi uliopita, matukio hayo yalijitokeza mara mbili.

Matokeo ya utafiti huo wa TGNP na Kituo cha Taarifa na Maarifa-Kata ya Mabogini, yaliwasilishwa mwishoni mwa wiki na Benard Massawe kwa Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Moshi, Lukas Mselle.

Mselle na timu yake ya baadhi ya wakuu wa idara za halmashauri hiyo, walipokea utafiti huo na kushauri baadhi ya mambo ambayo Kituo cha Taarifa na Maarifa kinapaswa kuongeza katika ripoti yao, ili kusaidia serikali kuchukua hatua.

Maeneo tishio kwa ukatili wa kingono, hasa ulawiti na ubakaji yametajwa ni vijiji vya Mserekia, Mabogini, Chekereni, Muungano na Maendeleo, huku ndoa za utotoni zikionekana kuwa mwiba zaidi eneo la Remiti, kijiji cha Mserekia.

Pamoja na mambo mengine, utafiti huo umebaini vijana hao huungana na kusubiri watu walewe pombe na baada ya hapo humchukua mtu huyo, ambaye wamepanga kwamba ni siku yake kulawitiwa na hufanya hivyo huku wakimrekodi kwa kumpiga picha jongefu (video).

"Kuna vijana wengi wanalawitiwa na wa kike wamekuwa wakibakwa katika maeneo hayo.

Wako wanafunzi wanaachishwa shule na kuozwa katika umri mdogo; umri ambao si sahihi kuolewa. Maeneo watoto wanaolewa ni Remiti, kijiji cha Mserekia. Maeneo hayo yamekuwa yanaathiriwa zaidi na ukatili huu.

"Wanafunzi wengi wamekuwa wakitoka majumbani kufuata elimu maeneo ya kijiji cha Chekereni, mahali penye umbali mrefu; ukizingatia watoto wanakutana na changamoto mbalimbali na huko kuna mapori katikati.

"Pia katika vijiji vyetu kumekuwa na ukatili unaotokana na matumizi makubwa ya dawa za kulevya, ikiwamo bangi na mirungi. Kijiji cha Mabogini kimeathiriwa na dawa hizi hasa kituo kidogo cha mabasi ya abiria cha Chekereni.

"Wakishatumia dawa za kulevya, wanakwenda kufanya ukatili wa kijinsia katika jamii zetu. Vijana wengi wamekuwa wakikutana maeneo hayo na biashara hizo zimekuwa zikiendelea na watumiaji wamekuwa wakipatikana maeneo hayo," alisema.

> **"Pia katika vijiji vyetu kumekuwa na ukatili unaotokana na matumizi makubwa ya dawa za kulevya, ikiwamo bangi na mirungi. Kijiji cha Mabogini kimeathiriwa na dawa hizi hasa kituo kidogo cha mabasi ya abiria...**

Kata ya Mabogini inaundwa na vijiji vya Mvuleni, Mji Mpya, Maendeleo, Chekereni, Muungano, Mabogini, Mtakuja na Mserekia.

Ofisa na Mwezeshaji wa TGNP, Agness Rukanga, alisema Halmashauri ya Wilaya ya Moshi ni kati ya halmashauri ambazo zina ukatili mkubwa, hasa kata ya Mabogini kutokana na kutajwa katika utafiti wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuwahudumia Watoto (UNICEF).

"Katika ngazi ya kata, tumepata mapokeo mazuri na ushirikiano mzuri sana na uongozi wa kata umeahidi baada ya kumalizika shughuli za uchaguzi wa serikali za mitaa, vijiji na vitongoji, wanatamani kukaa na kundi zima, ili kutafuta njia ya kutatua zile changamoto ambazo zimeibuliwa.

"Tupo hapa kujitambulisha kwamba TGNP tupo. Mjue tuna hiki kituo na mtashirikiana nao katika utendaji, hasa suala zima la bajeti katika mrengo wa kijinsia au katika uchambuzi wa miongozo, kanuni mbalimbali na jicho la kijinsia. Ninaamini watakuwa ni washiriki wazuri na kwa njia moja au nyingine wanaweza kuishauri halmashauri," alisema.

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Moshi, Mselle, akijibu hoja kuhusu utafiti huo, alisema yote yaliyoibuliwa atayafikisha kwa Mkurugenzi wake, Shadrack Mhagama, kwa kuwa serikali inaamini TGNP ni mkono wake wa pili, inawasaidia mambo mengi, hasa pale ambapo wameshindwa kufika, wao wanafanya.

"Mmeibua changamoto nyingi ambazo zinatukabili katika maeneo yetu. Kufahamu changamoto ni hatua ya awali ya namna ya kukabiliana na mambo yanayotukabili.

"Lengo likiwa ni kumhudumia mwananchi huyuhuyu, ambaye serikali ina dhamana ya kumhudumia. Ninyi wawakilishi wa kata ya Mabogini, niwapongeze kwa utayari wenu, kutoa muda wenu na kufanya haya mambo ambayo mmeyafanya.

"Mmefanya wasilisho zuri na kwa njia ya kitaalamu. Ni wazi kwamba walimu wenu Agness Rukanga na Happy Maruchu, walifanya kazi kubwa sana kuhakikisha kazi hii inafanyika," alisema.

Kwa mujibu wa Sheria ya Kanuni za Adhabu, Sura 16, kulawiti na kubaka/kunajisi kwa kundi ni kosa la jinai na adhabu yake ni kifungo cha maisha gerezani.

## Bandari ya Tanga yashughulikia meli kubwa baada ya uwekezaji bil. 429/-

**Na Mwandishi Wetu,** TANGA

UTENDAJI wa Bandari ya Tanga, umeimarika kwa kiasi kikubwa katika miaka ya hivi karibuni kutokana na uwekezaji wa serikali wa Sh. bilioni 429.1.

Bandari hiyo ilijengwa kwa mara ya kwanza mwaka 1914, ili kukidhi mahitaji ya kibiashara na kilimo kaskazini mwa Tanzania.

Ni bandari iliyopata uwekezaji mkubwa wa umma katika kipindi cha miaka mitano iliyopita na kuiweka katika ramani ya kimataifa, kama kituo muhimu kwa meli kubwa.

Meneja wa Bandari ya Tanga, Masoud Mrisha, aliwaambia waandishi wa habari waliotembelea bandari hiyo wiki hii kuwa, bandari hiyo imepata matokeo chanya matano kutokana na uwekezaji huo.

"Sasa tuna uwezo wa kushughulikia meli kubwa zaidi kuliko hapo awali," alisema.

Maboresho katika Bandari ya Tanga yalifanyika kwa awamu mbili, ni pamoja na kuongeza kina cha maji kutoka mita tatu hadi mita 13 na kupanua njia ya meli kugeuza.

Mradi wa Sh. bilioni 429.1 pia ulijumuisha ununuzi wa vifaa vipya vya kushughulikia mizigo na upanuzi wa gati mbili katika bandari hadi upana wa mita 450.

"Pamoja na maboresho haya, meli sasa zinaweza kuja moja kwa moja kwenye gati hizo, ambayo ni mabadiliko makubwa kutoka kwa hali ya awali ambapo meli zililazimika kufunga kwenye kina cha umbali wa kilomita 1.7 nje ya gati," alisema.

Aliongeza kuwa, "wakati huo ilibidi kuzihudumia meli hizo kwa kutumia meli ndogo za kubebea mizigo na maboya. Kutegemea meli ndogo na maboya kulisababisha TPA (Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania) kutoa ada ya dola 1.3 kwa tani, kwa mizigo yote iliyosafirishwa kupitia Bandari ya Tanga.

"Ada hii haipo tena kwa sababu meli ndogo na kubwa, sasa zinaweza kupewa huduma ipasavyo katika Bandari ya Tanga," alifafanua Mrisha.

Alisema maboresho hayo pia yameimarisha utendaji kazi wa Bandari ya Tanga, yakiwezesha bandari kupakua mizigo kutoka kwa meli kubwa ndani ya siku mbili, tofauti na siku tano au zaidi zilizokuwa zinahitajika awali.

Wakati wa robo ya kwanza ya mwaka wa fedha wa sasa, bandari hiyo ilihudumia jumla ya tani 333,643 za mizigo, ikipita lengo lake la tani 283,225 kwa asilimia 17.

"Hii ni uboreshaji mkubwa kulinganishwa na tani 204,000 zilizohudumiwa katika kipindi kama hicho mwaka wa fedha wa 2023/24. Kwa ujumla, Bandari ya Tanga ilishughulikia tani 1,191,480 za mizigo wakati wa mwaka mzima wa fedha wa 2023/24, ikiongezeka kutoka tani 890,901 mwaka uliopita.

"Aidha, bandari hii ilifanikiwa kuhudumia meli 113 wakati wa robo ya kwanza, ikipita lengo lake la kuhudumia meli tano tu. Mabadiliko haya yanaambatana na ununuzi wa vifaa vya kupakulia mizigo.

"Kwa ujumla, mabadiliko yanatarajiwa kuimarisha zaidi uwezo na ufanisi wa bandari katika kushughulikia mizigo ya baharini na kuchangia kwa namna chanya katika uchumi wa mkoa, kanda ya kaskazini na taifa kwa ujumla," alisema.





# Viongozi wawili BAVICHA, BAWACHA watimkia CCM

**Na Judith Julius,** NGARA

MWENYEKITI wa Baraza la Vijana Chama cha Demokrasia na Maendeleo CHADEMA (BAVICHA) Wilaya ya Ngara, Titho Philimon na Mwenyekiti wa Mwenyekiti wa Baraza la Wanawake CHADEMA (BAWACHA) wilayani hapa, Catherine James wamejiunga na Chama cha Mapinduzi (CCM) na kupokewa na Mwenyekiti wa Umoja wa Vijana wa chama hicho taifa, Mohamed Kawaida.

Wakizungumza wakati wa kuhama chama hicho juzi, viongozi hao walidai walifikia uamuzi huo kutokana na kuwa katika chama chao bila maendeleo yoyote.

Mwenyekiti wa BAVICHA, Philimon alisema aliamua kwenda CCM baada ya kuridhishwa na utendaji kazi wa Rais Samia Suluhu Hassan na kuwa hatua hiyo itamuwezesha kuungana na vijana wenzake wa kitanzania zaidi ya milioni 21.3 ili kufikia chachu ya maendeleo.

Naye Mwenyekiti BAWACHA Wilaya, Catherine alisema amekuwa kiongozi wa chama hicho kwa miaka 20, lakini haoni mafanikio ndani ya chama hicho.

**Alisema na barabara ambazo zitafanyiwa matengenezo zina urefu wa kilomita 716.64, ujenzi wa makalvati 381, madaraja manne, mitaro yenye urefu wa kilomita 5.28 na ujenzi wa barabara ...**

Aidha, alisema katika muda wake ndani ya chama hicho amejizolea wanachama zaidi ya 5,000 hivyo kumuhakikishia Kawaida kuwa watamfuata CCM na kuwa wote watakuwa tayari kutumika kwa muda wowote iwe mvua au jua, kwa maana wamedhamiria kumuunga mkono Rais Samia, hasa katika miradi mikubwa anayoitekeleza ndani ya wilaya ya Ngara. Akiwakaribisha ndani ya CCM, Mwenyekiti wa UVCCM Taifa, Kawaida aliwapongeza viongozi hao na kwa uamuzi wao na kusema kuwa wanaendelea na kauli mbiu yao isemayo wanazima zote wanawasha kijani.

Katika hatua nyingine, aliwataka viongozi wa vyama vya siasa kuacha kuwabeza viongozi na wasimamizi wa uandikishaji wa daftari la wakazi, kwa ajili ya kushiriki Uchaguzi wa Serikali za Mitaa na kuwataka kuwa sehemu ya uhamasishaji wanachama kushiriki hatua zote na siyo kulalamikia juhudi zinazofanywa.



Mkuu wa Mkoa wa Mara, Kanali Evans Mtambi (mwenye suti ya bluu na kofia), akiwasikiliza wakazi wa Kata ya Nyatwali wilayani Bunda juzi, alipokwenda kufuatilia uhamishaji wa watu, ili kupisha eneo hilo, kwa ajili ya Hifadhi ya Mbuga ya Serengeti. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# KASHWASA yaelemewa na madeni ya mamlaka

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

KITUO cha uzalishaji maji katika mikoa sita Mwanza, Shinyanga, Simiyu, Singida, Geita na Tabora cha Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Shinyanga na Kahama (KASHWASA) kilichoko Ihelele, wilayani misungwi mkoani Mwanza, kimetajwa kuwa hatarini kushindwa kujiendesha kutokana na kuzidai mamlaka za maji katika mikoa hiyo zaidi ya Sh. bilioni 15.

Kituo hicho kinachotegemewa zaidi kupeleka maji ya Ziwa Victoria katika mikoa ya Singida na Dodoma, undeshwaji wake unatajwa kuwa hatarini kutokana na mamlaka zinazouziwa maji hayo kushindwa kulipa madeni yake.

Akizungumza wakati wa ziara ya Mkuu wa Mkoa wa Tabora, Paul Chacha kituoni hapo, Meneja Huduma kwa Wateja KASHWASA, John Zengo, alisema hadi kufikia Septemba 30 mwaka huu, wanadai Sh. bilioni 15 kwenye mamlaka za maji ambazo huwa wanaziuzia maji hayo ya Ziwa Victoria kwa jumla. Aidha, alisema hali hiyo inakwamisha utekelezaji wa majukumu na mahitaji mbalimbali kituoni hapo, ikiwa ni sehemu ya kituo hicho kujiendesha chenyewe bila kutegemea fedha kutoka serikalini.

Alisema mradi huo wa maji ya Ziwa Victoria, ulianzishwa mwaka 2003 na kukamilika 2008, na 2009 ndipo KASHWASA ikaundwa na kuanza kuuza maji ya jumla kwenye mamlaka mbili za Kahama na Shinyanga, na walikuwa wakizalisha maji kwa siku lita milioni 18 na kuwa sasa hivi una hudumia mikoa sita ya Mwanza, Shinyanga, Simiyu, Singida, Geita na Tabora.

"Mradi huu una uwezo wa kuzalisha maji kwa siku lita milioni 80 na baadhi ya miundombinu inaweza kupanuliwa na kuongeza uwezo wa kuzalisha maji hadi kufikia lita milioni 120 kwa siku, lakini kulingana na uhitaji sasa hivi katika mikoa sita tunazalisha lita milioni 72 kwa siku kutoka milioni 18." alisema John.

Kadhalika, alitaja uharibifu wa mazingira kwa wananchi kufanya shughuli za kibinadamu kwenye madakio ya maji ya Ziwa Victoria, na kusababisha matope kuwa mengi hasa msimu wa mvua, na kuingia gharama kubwa ya kutibu maji na kusababisha uzalishaji wa maji kuwa mdogo.

Baada ya kupokea taarifa hiyo, Mkuu wa Mkoa wa Tabora Paul Chacha, alionesha kusikitishwa na ukubwa wa madeni hayo na kutaja hali hiyo kuwa ni hatari kwa mradi huo wa maji ya Ziwa Victoria na kuwa baadaye unaweza kushindwa kujiendesha kutokana na ukosefu wa fedha.

"Wekeni nguvu kudai madeni hayo, vinginevyo mtasuasua katika uendeshaji wa mradi, na mimi katika Mkoa wangu wa Tabora nitawasaidia kudai madeni yenu kwenye Mamlaka za Maji, nitakaa nao na kuwekeana mikakati ya kulipa madeni yote ili tusije kuua mradi huu,"alisema Chacha.

Baadhi ya wajumbe wa kamati ya ulinzi na usalama kutoka Tabora, wakizungumza katika majadiliano, waliishauri KASHWASA, kwamba katika eneo la utunzaji mazingira ni vyema wakaweka alama kwenye mipaka yao, ili kulinda maeneo yasivamiwe na wananchi, pamoja na kufanya doria za mara kwa mara wakishirikiana pia na ofisi ya mkuu wa wilaya.

## Usajili wa mikopo asilimia 10 kwenye mfumo kuanza rasmi

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

USAJILI kupitia mfumo mpya wa kidijitali kwa vikundi vya vijana, wanawake na wenye ulemavu vinavyonufaika na mikopo ya asilimia 10 ya halmashauri, unatarajiwa kuanza kutumika baada ya mikopo hiyo kuruhusiwa kutolewa tena lengo likiwa ni kudhibiti mianya ya udanganyifu iliyotajwa kujitokeza hapo awali.

Akizungumza wakati wa kuhitimisha mafunzo ya matumizi ya mfumo huo mpya kwa maaofisa maendeleo ya jamii kutoka kata 18, Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri ya Msalala, mkoani Shinyanga, Mary Nziku alisema tayari wametenga Sh. bilioni 1.08 kwaajili ya mikopo hiyo.

Alisema zinalenga kuwasaidia kukuza uchumi na kuondokana na kuingia kwenye mikopo umiza inayosababisha wengi kukimbia familia zao na kupoteza malengo yao binafsi.


Alisema kupitia mfumo huo mpya kutakuwa na uwazi na utambuzi wa vikundi na wanavikundi waliochukua mikopo na uendelevu wa shughuli zao ili kurahisishwa urejeshwaji wa mikopo hiyo.

Nziku alisema kila kikundi kinatakiwa kuwa na shughuli ya kufanya ambayo inawaingizia kipato, kwani lengo la utoaji wa fedha hizo ni kukuza mitaji iliyopo na sio kuibua biashara mpya na mwisho kushindwa kurejesha kwa wakati na kuvinyima fursa vikundi vingine kukopa kwasababau zinatolewa kwa awamu na sio mkupuo.

Ofisa Maendeleo ya Jamii Kata ya Mwaluguru, Julius Sungura alisema mfumo huo utasaidia kuwaondoa kwenye lawama zilizokuwa zikitolewa na wanavikundi kuwa wanapendelea na sasa vikundi vinaweza kujisajili wenyewe kwenye mfumo na hakutakuwepo mikopo yenye ujanja ujanja nakutimiza adhima ya Rais kwa makundi yote kunufaika. Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Mboni Mhita alisema ofisa maendeleo ya jamii ndiyo wasimamizi wakuu wa fedha hizo wamepewa mafunzo, ili kuimarisha vikundi na kusiwepo kikundi hewa kama ilivyokuwa miaka iliyopita.

Mhita alisema mfumo wa zamani ulikuwa wakusajili kwa kuandika majina kwenye karatasi huku baadhi ya vikundi vingine kutokuwepo na vingine kushindwa kurejesha kwa utaratibu, kwa sasa hakuna kikundi kitakachopotea hewani au kutorejesha kwakuwa vitakuwa vimesajiliwa kwenye mfumo huo maalam.

Nipashe
Spotika




WACHEZAJI MAJERUHI TANGU UKOSOAJI ONGEZEKO LA RATIBA UK. 12-13



# HIZI NDIZO REKODI ZA TUCHEL, KOCHA MPYA WA ENGLAND

**LONDON,** England

THOMAS Tuchel, ameteuliwa kuwa kocha mpya wa England akichukua mikoba ya Gareth Southgate.

Tuchel amekuwa kocha wa tatu wa kigeni kuinoa England na Mjerumani wa kwanza kuchukua mikoba ya 'Simba Watatu' hao, huku alitarajiwa kuanza kazi yake mwanzoni mwa 2025.

Kocha huyo wa zamani wa Chelsea na Bayern Munich, ana jukumu la pekee la kuipa England Kombe lao la Dunia kwa mara ya kwanza tangu 1966.

Akiwa amebarikiwa kwa ujuzi wa hali ya juu wa mbinu na uwezo wa kurekebisha kanuni zake kwa msingi wa mchezo baada ya mchezo, ili kubatilisha wapinzani, Tuchel amejizolea sifa ya kuwa mtaalam wa soka la mtoano.

Orodha yake ya heshima inathibitisha hilo. Ikiwa wewe ni mmoja wa wachache ambao labda wana shaka kuhusu uteuzi wa Tuchel, data za hapa chini zinaweza kusaidia kubadilisha maoni yako.

Huu hapa ni muhtasari wa rekodi ya kocha mpya wa England katika mechi za mtoano...

Tuchel anaweza kuwa hana uzoefu wa usimamizi wa kimataifa, lakini amefunzwa katika mazingira yenye shinikizo nyingi ambapo kushinda ndio njia pekee ya kutuliza.

Rekodi yake katika mechi za mtoano ni nzuri, huku Mjerumani huyo akishinda zaidi ya asilimia 70 ya mechi kama hizo.

Kiwango cha ushindi wa asilimia 50 katika mechi za hatua ya mtoano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, ndicho cha chini zaidi katika mashindano yote ambayo amesimamia, lakini idadi hiyo inaheshimika kutokana na kiwango cha upinzani.

Tuchel ameshinda mechi 15 kati ya 30 za hatua ya mtoano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya na kuziongoza timu mbili hadi fainali na kubeba kombe hilo mara moja, akiwa na Chelsea mnamo 2021 kutoka nyuma ya safu ngumu ya ulinzi.

PSG ya Tuchel ilifungwa na Bayern Munich, washindi wote katika fainali ya 2020, huku 'uchawi' wa Real Madrid ukimzuia Mjerumani huyo kutinga fainali ya tatu ya Ligi ya Mabingwa mwaka 2023.

Timu yake ya Chelsea, ikiwa ni mabingwa, ilikuwa kwenye ukingo wa kuishinda Madrid kwenye Uwanja wa Santiago Bernabeu na kutinga nusu fainali, baada ya kupindua matokeo ya 3-1 katika mechi ya mkondo wa kwanza, lakini mabao matatu ya Luka Modric yalichochea pambano la kuvutia la Madrid.

Bado, ushindi huo katika mji mkuu wa Hispania ulionesha zaidi uwezo wa Tuchel katika mechi za mtoano.

Amesimamia kampeni moja pekee ya Ligi ya Europa - mnamo 2015/16 akiwa na Borussia Dortmund - ambayo ilijivunia ahadi nyingi kabla ya timu yake kushindwa pale Anfield na Liverpool katika nane bora.

### LIGI ZA NDANI

Tuchel amepata mafanikio makubwa katika mashindano ya mataji, lakini si kila mara amepata timu yake kwenye mstari.

Mjerumani huyo aliiwezesha Chelsea kutinga fainali mbili za Kombe la FA, ambapo zote walipoteza, fainali ya Kombe la Carabao, ambayo walifungwa na Liverpool kwa mikwaju ya penalti.

Borussia Dortmund ilifika fainali mbili za DFB-Pokal, wakishinda taji la kwanza la klabu hiyo, baada ya Jurgen Klopp.

Na kule PSG alitinga fainali mbili za Coupe de France na kupoteza moja kwa Rennes kwa mikwaju ya penalti.

Bado, viwango vyake vya ushindi katika mashindano yaliyotajwa hapo juu na vile vile Coupe de la Ligue ni zaidi ya asilimia 73.

Ingawa Tuchel anaonekana kujivunia nafasi nzuri ya kusonga mbele katika mchuano yoyote, ni jambo la kutatanisha ikiwa ataifikisha timu yake kwenye mstari, haswa ikiwa pambano linakwenda kwa mikwaju ya penalti.

Ukiondoa Super Cup na wachezaji wengine wote wa nyumbani, Tuchel amefanikiwa katika fainali 11 kuu na kushinda tano kati ya hizo.

Nusu ya kushindwa kwake sita alitolewa kupitia mikwaju ya penalti, ikiwa ni pamoja na mbili nchini England.

### ISIKUPITE



ARSENAL ndiyo klabu inayoongoza kwa wachezaji wake kutolewa nje kwa kadi nyekundu hadi sasa msimu huu, hii ni baada ya William Saliba kulimwa 'umeme' juzi wakati wakichezea kichapo cha mabao 2-0 dhidi ya Bournemouth.

Nyekundu hiyo kwa Saliba ni ya kwanza kwake katika historia yake ya soka, wachezaji wengine wa Arsenal waliokula 'umeme' msimu huu ni Declan Rice na Leandro Trossard.

# WACHEZAJI MAJERUHI TANGU UKOSOAJI ONGEZEKO LA RATIBA



ALISSON

**LONDON,** England

WACHEZAJI wa soka wamekuwa wakikosoa kalenda ya mechi katika miezi ya hivi karibuni, huku mashindano ya klabu na mashindano ya kimataifa yakiboreshwa na kuongezwa ukubwa.

**Huku Uefa ikibadilisha muundo wa Ligi ya Mabingwa Ulaya, Ligi ya Europa na Ligi ya Europa Conference pamoja na FIFA kupanua Kombe lake la Dunia na Kombe la Klabu Bingwa Dunia, wachezaji wameanza kuelezea wasiwasi wao juu ya kile wanachoamini ni kupanda kusiko endelevu kwa ratiba.**

Baadhi ya nyota wakubwa wa mchezo huo wamezungumza juu ya ratiba ngumu na kupunguzwa kikatili na majeraha ya umuhimu tofauti, mara baada ya hapo. Ingawa umuhimu wa Rodri kwa Manchester City, uliripotiwa sana baada ya kupata jeraha la mguu lililoisha msimu uliopita, si mwanasoka pekee aliyepona akiwa nje ya uwanja baada ya kufunguka kuhusu ongezeko la mahitaji.

Hapa kuna baadhi ya nyota ambao wamekuwa hawana bahati ambao wamehitaji muda kwenye meza ya matibabu hivi karibuni...

### 1. RODRI

Kiungo wa kati wa Man City na Hispania, Rodri alionekana kuwa msemaji asiye rasmi wa wanasoka alipolenga kuongeza mzigo wa kazi Septemba.

Mshindi huyo wa Euro 2024, alifichua kuwa wachezaji wamechoshwa na kukiri kwamba kulikuwa na mazungumzo ya uwezekano wa kugoma.

Alisema: "Ndiyo, nadhani tunakaribia kugoma. Ikiendelea hivi hatutakuwa na chaguo lingine. Ni jambo ambalo linatutia wasiwasi.

"Kati ya 40 na 50 ni kiasi cha michezo ambayo mchezaji anaweza kucheza kwa kiwango cha juu zaidi. Baada ya hapo unashuka kwa sababu haiwezekani kuendeleza kiwango cha kimwili. Mwaka huu tunaenda hadi 70 au labda 80. maoni yangu ya unyenyekevu, nadhani ni nyingi sana."

Rodri alithibitishwa kuwa sahihi kwa njia ya kutisha alipoanguka wakati City ilipokutana na wapinzani wa Ligi Kuu England, Arsenal. Hatarajiwi kucheza tena msimu huu.

### 2. SON HEUNG-MIN

Nahodha wa Tottenham Hotspur, Son Heung-min pia amekaa nje ya uwanja hivi majuzi, ingawa jeraha lake si baya sana kama Rodri, kwani mwishoni mwa wiki alirejea uwanjani.

Raia huyo wa Korea Kusini, alikiri mwezi uliopita kuwa hahisi kuwa wachezaji wanatunzwa, huku baadhi ya wachezaji wa ngazi za juu wa kimataifa wakiwa katika hatari ya kucheza katika takriban mechi 85 msimu huu.

Akizungumza kwenye kongamano la mashabiki, Son alisema: "Hatuwezi kuidhibiti. Tunahisi hatuchungwi mtu anapokwenda kwenye Euro, ana likizo ya wiki mbili tu na kurejea kwenye maandalizi ya msimu mpya, ili kuanza msimu. Hii ni kali.

"Kwa kweli tunahitaji kufanya mabadiliko, ndio. Tunachotaka kuona ni michezo ya ubora, si michezo mingi iwezekanavyo. Ikiwa michezo ni mingi kama ilivyo sasa, wachezaji watakuwa majeruhi, hawatacheza vizuri na nadhani hii si ya kuombea kuona.

"Kwa hakika tunahitaji kubadilisha kitu na wachezaji wanatakiwa kujitokeza na kusema kitu."

Son alitoka na malalamiko katika ushindi wa mabao 3-0 wa Ligi ya Europa dhidi ya Qarabag na hajaonekana tangu wakati huo, ingawa kurudi kunafikiriwa kuwa karibu.

### 3. ALISSON

Nyota mwingine bora wa Ligi Kuu ya England, kipa wa Liverpool, Alisson amekuwa na majeraha mengi katika miaka ya hivi karibuni. Alipata shida nyingine kabla ya mapumziko ya kimataifa na Mbrazil huyo anatarajiwa kuwa fiti Novemba.

Kwa mara nyingine tena, jeraha hilo lilikuja muda mfupi baada ya mlinda mlango kuangazia ongezeko la mahitaji, hasa akilenga Ligi ya Mabingwa Ulaya iliyoboreshwa ambayo sasa inahusisha mechi nane za 'awamu ya ligi' badala ya hatua ya makundi.

Alifichua: "Wakati mwingine hakuna mtu anayewauliza wachezaji wanafikiri nini kuhusu kuongeza michezo zaidi kwa hivyo, labda maoni yetu haijalishi. Lakini kila mtu anajua tunachofikiria kuhusu kuwa na michezo mingi. Kila mtu amechoshwa na hilo.

"Sisi si wajinga, tunaelewa kuwa watu wanataka michezo zaidi, lakini jambo la busara lingekuwa kwa watu wote niliowataja - wale wanaounda kalenda - kukaa pamoja na kuwasikiliza wachezaji.

"Nataka kutoa ubora katika michezo yote ninayocheza, lakini tunahitaji suluhu. Haionekani kuwa tunakaribia suluhu nzuri kwa ajili ya soka na wachezaji."

### 4. DANI CARVAJAL

Mshindi wa Ligi ya Mabingwa Ulaya na Euro 2024, Dani Carvajal anaweza kuwa katika hatari ya kucheza idadi kubwa ya michezo hatari, ikizingatiwa anachezea Real Madrid na Hispania, timu mbili zinazotawala katika michuano kimataifa.

Hata hivyo, beki huyo wa kulia ni nyota mwingine ambaye amepata jeraha la mguu, huku mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 32, akichelewa kufika kwenye pambano la LaLiga dhidi ya Villarreal.

"Nadhani ukimuuliza mwanasoka yeyote, atakuambia jambo lile lile. Si maoni ya Rodri pekee," nyota huyo wa Real Madrid alisema.

"Nadhani ni maoni ya wachezaji na hili likiendelea, itafika wakati kutakuwa hakuna njia nyingine, sijui nini kitatokea, lakini ni jambo ambalo linatutia wasiwasi kwa sababu sisi ndio tunateseka."

Mkataba wa Carvajal ulikuwa unamalizika majira ya joto, lakini Madrid wamefanya jambo la hali ya juu na kurefusha hadi 2026.

### 5. JURRIEN TIMBER

Jurrien Timber, alipata jeraha la mguu wikiendi ya ufunguzi wa msimu wa 2023/24, lakini anashukuru kupata michezo zaidi mwanzoni mwa kampeni ya sasa. Mchezaji huyo wa kimataifa wa Uholanzi, alikiri kuwa ana furaha kucheza baada ya kurejea kwenye pambano la siku ya mechi, lakini akakubali kwamba wenzake wana pointi.

Hivi majuzi alisema: "Ni mada kubwa kwa sasa katika vyumba vya kubadilishia nguo, si tu kwa Man City na Liverpool bali pia chumba chetu cha kubadilishia nguo.

"Sikucheza msimu uliopita, kwa hiyo ninafurahia kucheza hivi sasa - hautanisikia nikilalamika - lakini ninaelewa kabisa kile wanachosema."

Akijibu alipoulizwa kama wachezaji wako katika hatari zaidi kwa sababu ya kalenda, Mholanzi huyo aliongeza: "Bila shaka. Ninafikiri ni jambo la hatari. Wiki iliyopita tulicheza na City na nadhani walicheza tena siku mbili baadaye - hiyo ni kubwa mno..."

Timber kwa sasa ana tatizo la misuli hali iliyomlazimu kukosa katika ushindi wa mabao 3-1 wa Arsenal dhidi ya Southampton kabla ya mapumziko ya kimataifa, lakini hatarajiwi kukosekana kwa muda mrefu zaidi.

## Nukuu

"Lazima kubadilika, ni wazi kabisa kwamba hawatapata pointi za kutosha ikiwa haitawezekana - umeona michezo ambayo imefanyika tayari msimu huu na sare mbili na kushindwa huku. Haiwezi kuendelea," **Mchambuzi wa soka na mshambuliaji wa zamani wa Newcastle na England, Alan Shearer, akiitaka Arsenal kudumisha nidhamu zaidi uwanjani baada ya William Saliba, juzi kuwa mchezaji wa tatu wa klabu hiyo msimu huu kutolewa nje kwa kadi nyekundu.**



"Ni mtaalamu wa hali ya juu na mtu mzuri. Ni furaha kumfundisha [Luka] Modric, kufanya kazi naye. Kila kitu ambacho ameweza kufikia na anafanikiwa, anastahili," **Kocha wa Real Madrid, Carlo Ancelotti, akimpa maua yake Modric (39), wakati alipoweka rekodi ya kuwa mchezaji mwenye umri mkubwa zaidi kuwahi kuichezea timu hiyo, juzi wakishinda 2-1 ugenini dhidi ya Celta Vigo.**




"Inapendeza sana kucheza hapa nikihisi mapenzi ya mashabiki wa Argentina, inanitia hisia kuwasikiliza jinsi wanavyopiga kelele jina langu. Sote tunafurahia uhusiano huu na mashabiki na tunapenda kucheza nyumbani. Sikuweka tarehe ya mwisho kuhusu mustakabali wangu, kwa sababu najua hii inaweza kuwa michezo yangu ya mwisho," **Lionel Messi baada ya wiki iliyopita kuiongoza Argentina kushinda 6-0 dhidi ya Bolivia kuwania kufuzu Kombe la Dunia 2025, Ukanda wa Amerika Kusini.**



# YALIYOJIRI 'DABI' SIMBA, YANGA KATIKA NAMBA




Straika wa Simba, Leonel Ateba, akijaribu kumpiga chenga kipa wa Yanga, Djigui Diarra, kwenye mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara kati ya timu hizo mbili uliochezwa juzi, Uwanja wa Benjamin Mpaka, Dar es Salaam. Yanga ilishinda bao 1-0. **MPIGAPICHA WETU**

**Na Adam Fungamwango**

MECHI ya watani wa jadi, Simba na Yanga ilimalizika Jumamosi iliyopita, kwa Yanga kupata ushindi wa bao 1-0, ambapo beki wa kulia wa 'Wekundu wa Msimbazi', Kelvin Kijili, alijifunga mwenyewe katika harakati za kutaka kuokoa.

**Ilikuwa ni mechi ya raundi ya nane ya Ligi Kuu Tanzania Bara, mzunguko wa kwanza iliyochezwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.**

Katika makala haya, tunakuletea matukio, takwimu, rekodi na yote ya kusisimua yaliyojiri kwenye mchezo huo, twende sasa...

**86#** Ni dakika ambayo Yanga ilipata bao la ushindi kwenye mchezo huo, ambalo beki wa Simba, Kelvin Kijili, alijifunga mwenyewe alipokuwa akijaribu kuokoa.

**70#** Ni dakika ambayo beki Chamou Karaboue aliyeingia badala ya Abdurazack Hamza, aliteleza akiwa karibu na lango lake, baada ya kupasiwa mpira na Moussa Camara, mpira ukanaswa na wachezaji wa Yanga, lakini kipa wa Simba akisimama imara na kuokoa.

**64#** Ni namba ya mchezo huo kwa mujibu wa Bodi ya Ligi katika mpangilio wao wa michezo yote ya Ligi Kuu Tanzania Bara msimu wa 2024/25.

**42#** Ni dakika ambayo Yanga ilifanya shambulio pekee la hatari zaidi katika kipindi cha kwanza, mpira wa Pacome Zouzoua aliurudisha ndani wachezaji wa Simba wakidhani ulikuwa umetoka, ulimkuta Stephane Aziz Ki, aliyepiga shuti kali akiwa karibu na lango, lakini ulidakwa na kipa Camara kisha ukamponyoka na kugonga nguzo ya pembeni, kabla ya kuudaka tena.

**37#** Abdulrazack Hamza, angeweza kuipatia Simba bao katika dakika hii, lakini mpira aliounganisha kwa kichwa kutokana na faulo ya Jean Charles Ahoua, ulipaa juu lango.

**29#** Namba hii inasimama kama idadi ya michezo ambayo timu hizo zimekutana tangu msimu wa Ligi Kuu 2010/11.

**27#** Ni dakika ambayo mchezaji wa Yanga, Stephane Aziz Ki, alikaribia kuiandikia Yanga bao, shuti lake lilimbabatiza Fondoh Che Malone, mpira ukampoteza maboya kipa, Camara, lakini bahati nzuri ulitoka nje.

**13#** Ni dakika ambayo Yanga ilifika kwa mara ya kwanza kwenye lango la Simba, baada ya wapinzani wao kuanza mchezo huo kwa kasi na kukosa mabao mawili ya wazi dakika za mwanzoni.

**10#** Yanga ilichezesha jumla ya wachezaji 10 wa kigeni katika mchezo wao dhidi ya Simba, ambao ni Djigui Diarra raia wa Mali, Yao Kouassi na Pacome Zouzoua kutoka Ivort Coast, Shadrack Boka na Maxi Nzengeli (Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo), Khalid Aucho ambaye ni Mganda, Prince Dube (Mzimbabwe), Stephane Aziz Ki (Burkina Faso), Wazambia Kenneth Musonda na Clatous Chama.

Namba hii pia inasimama kama idadi ya michezo ambayo Yanga imeifunga Simba kwenye michezo ya Ligi Kuu tangu msimu wa 2010/11.

**9#** Idadi ya wachezaji wote wa Simba wa kigeni waliocheza kwenye mchezo wa juzi, nao ni Moussa Camara raia wa Mali, Fondoh Che Malome na Leonel Ateba (Cameroon), Debora Fernandes (Angola), Jean Charles Ahoua na Chamou Karaboue (Ivory Coast), Joshua Mulate (Zambia), Steven Mukwala (Uganda) na Augustine Okajepha wa Nigeria.

**8#** Yanga ilianzisha idadi hii ya wachezaji wa kigeni katika mchezo wa jana, ambao ni Djigui Diarra raia wa Mali, Yao Kouassi na Pacome Zouzoua (Ivort Coast), Shadrack Boka na Maxi Nzengeli (DR Congo), Khalid Aucho (Uganda), Prince Dube (Zimbabwe), Stephane Aziz Ki ambaye ni raia wa Burkina Faso.

**7#** Jumla ya wachezaji wote wazawa wa Simba ambao walicheza mchezo wa juzi, dhidi ya Yanga ambao ni Shomari Kapombe, Mohamed Hussein, Abdulrazack Hamza, Yusuph Kagoma, Kibu Denis, Kelvin Kijili na Edwin Balua.

**6#** Ni idadi ya wachezaji wa kigeni ambao Simba iliwaanzisha katika mchezo wa Jumamosi, nao ni Moussa Camara raia wa Mali, Fondoh Che Malome na Leonel Ateba (Cameroon), Debora Fernandes (Angola), Jean Charles Ahoua (Ivory Coast) na Joshua Mulate wa Zambia.

**5#** Idadi ya wachezaji wote wa Yanga wazawa waliocheza mechi ya watani wa jadi dhidi ya Simba Jumamosi, iliyopita ambao ni Dickson Job, Mudathir Yahaya, Ibrahim Hamad 'Bacca', huku Clement Mzize na Bakari Mwanyeto wakiingia kipindi cha pili kutokea benchini.

**4#** Leonel Ateba alikosa bao la wazi kwenye dakika hii, alipojaribu kumlamba chenga Diarra, lakini kipa huyo alikuwa makini na kuondosha hatari.

**3#** Namba hii inasimama kwa wachezaji watatu wa Yanga wazawa walioanza mchezo wa dabi, ambao ni Dickson Job, Mudathir Yahaya na Ibrahim Hamad 'Bacca'.

**2#** Idadi ya makipa wa kigeni waliodaka mchezo huo, Diarra kwa upande wa Yanga na Camara upande wa Simba.

**1#** Bao pekee lilopatikana katika mchezo huo, uliopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam, ambalo liliipa Yanga pointi tatu.

## JE, WAJUA?



LUKA Modric (39), amewekа rekodi ya kuwa mchezaji mwenye umri mkubwa zaidi kuwahi kuicheza Real Madrid, wakati timu yake ikishinda mabao 2-1 ugenini dhidi ya Celta Vigo kwenye LaLiga juzi.





## Shirika latoa mikono saidizi kusaidia waliopoteza viungo

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

SHIRIKA la The Hand Project kutoka nchini Ujerumani, limetoa mikono saidizi 100 katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Dodoma, ili kuwasaidia watu waliopoteza viungo hivyo.

Akizungumza jana wakati wa hafla ya kukabidhi viungo hivyo, Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule, alisema mikono hiyo itawasaidia watu kuendelea na shughuli zao za kiuchumi.

"Ninalishukuru sana shirika hili kutokana na msaada waliotoa, hii inaonesha jinsi gani mpo pamoja na serikali kwa ajili ya kuinua sekta ya afya nchini.

"Ni furaha kuona jamii iliyopoteza matumaini ikirudishiwa tena tabasamu kwa kuwekewa viungo hivi ambavyo vitawasaidia kufanya kazi zao za kila siku," alipongeza.

Hata hivyo, Mkuu wa Mkoa alisema kuna haja wataalamu wa ndani kujengewa uwezo wa kutengeneza viungo saidizi hivyo, ili kusaidia kukidhi mahitaji ya viungo hivyo kwa jamii inayowazunguka.

Mganga Mkuu wa Mkoa huo, Dk. Thomas Rutachunzibwa, alishukuru serikali kwa kushirikiana na wadau wa afya kuleta kambi za huduma za matibabu bila malipo.

Alisema kambi ya sita imefanyika ndani ya mkoa huo kwa miezi miwili, ambapo wametoa huduma mbalimbali za kibingwa kwa wananchi.

Mratibu wa Hand Project nchini (mkoani Arusha), Veronica Kidemi ambaye pia ni mnufaika wa mkono saidizi, alisema shirika hilo limekuwa likisaidiana na wadau mbalimbali kuinua sekta ya afya nchini.

Alisema shirika hilo limeungana na serikali kutoa huduma kwenye hospitali za serikali na mikono inayotolewa ni ya aina tofauti, ikiwamo ya urembo kwa ajili ya kutembelea na ya kufanyia kazi.

Alisema kuwa jamii kupatiwa huduma hiyo ya viungo saidizi, itawasaidia kufanya shughuli zao za kujiinua kiuchumi na kuwaepusha kuwa tegemezi.

# Maelekezo saba yatolewa kuimarisha uzingatiaji maadili utumishi wa umma

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imetoa maelekezo saba kwa watumishi wa umma, baada ya kubaini kupungua kwa kiwango cha uzingatiaji maadili ya utendaji na kitaaluma kwenye maeneo ya kazi.

Katibu Mkuu Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Juma Mkomi, alitoa maelekezo hayo mwishoni mwa wiki jijini hapa, alipofunga kikao kazi cha kubadilishana uzoefu baina ya ofisi hiyo, taasisi simamizi za maadili na mamlaka zinazosimamia maadili kitaaluma.

Alisema maelekezo hayo ni pamoja na kuhakikisha masuala ya maadili yanakuwa sehemu ya usaili kwa wasailiwa wote na sehemu ya mafunzo elekezi kwa waajiriwa wapya wote katika utumishi wa umma.

"Pia hakikisheni kanuni za maadili ya utendaji katika utumishi wa umma pamoja na miongozo mingine ya maadili inapatikana kwa watumishi wote wanapoingia katika utumishi wa umma na miongozo hiyo kuwekwa kwenye tovuti rasmi za ofisi," aliagiza.

Mkomi aliwataka waendelee kufanya tathmini kwa kina kuhusu utendaji wa kimaadili (tabia na mienendo) kwa watumishi wakati wote, ili kuzishauri mamlaka ipasavyo. "Nendeni mkaimarishe matumizi ya TEHAMA katika utoaji huduma, ili kushughulikia mrejesho wa wananchi na kupunguza mazingira ya vitendo vya rushwa mahali pa kazi, pia imarisheni mifumo madhubuti na taratibu za kuwalinda watoa taarifa juu ya vitendo vya ukiukwaji maadili na rushwa mahali pa kazi," alielekeza.

> **"Ninawaelekeza mtumie matokeo ya utafiti na tathmini mbalimbali zinazofanyika kuhusu hali ya uadilifu na mapambano dhidi ya rushwa katika maeneo yenu ya kazi na utumishi...**

Pamoja na hayo, kiongozi huyo aliagiza hatua zichukuliwe dhidi ya watumishi wa umma wanaothibitika kukiuka maadili ya utumishi wa umma na kujihusisha na vitendo vya rushwa. "Ninawaelekeza mtumie matokeo ya utafiti na tathmini mbalimbali zinazofanyika kuhusu hali ya uadilifu na mapambano dhidi ya rushwa katika maeneo yenu ya kazi na utumishi wa umma kwa ujumla.

"Taarifa na uzoefu mnaobadilishana kupitia vikao kazi hivi, ili kutengeneza vihatarishi, afua na viashiria vya matokeo kuendana na mazingira yenu ya kazi, ziwe sehemu ya utekelezaji Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa Awamu ya Nne (NACSAP IV, 2023-2030)," aliagiza.

Awali alitaja changamoto zinazosababisha kupungua maadili hayo kuwa ni, kuajiri watumishi wapya bila kufanya upekuzi wa kutosha wala kuwafanyia upekuzi wa kutosha kuhusu tabia na mienendo kulingana na majukumu na miiko ya taaluma zao.

Alisema shida nyingine ni kutokuwa na mifumo madhubuti na taratibu za kuwalinda watoa taarifa juu ya vitendo vya ukiukwaji wa maadili na rushwa mahali pa kazi.




Hawa Mbura (aliyevaa miwani), akiwa na wanafunzi wa kike wa shule ya sekondari Kisasa katika picha ya pamoja, baada ya kutoa msaada wa taulo za kike kwa wasichana wa shule hiyo kwenye mahafali ya kidato cha nne yaliyofanyika mwishoni mwa wiki. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# TIRA kuendesha msako vyombo vya moto, vituo mafuta visivyokata bima

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MAMLAKA ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA) Kanda ya Kati, kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi, wamepanga kufanya operesheni ya ukaguzi wa vyombo vya moto na vituo vya mafuta ambavyo havijakatiwa bima kwa mujibu wa sheria.

Meneja wa TIRA wa Kanda hiyo, Frank Shangali, alibainisha hayo juzi jijini hapa wakati wa kikao na kampuni zinazotoa huduma za bima mkoa wa Dodoma kilichokuwa na lengo la kujadili mikakati ya kuongeza idadi ya watu wanaokata bima, kwa ajili ya mali na majanga mbalimbali.

Alisema kikao hicho ambacho kimejumuisha watoa huduma za bima mkoa wa Dodoma, kinalenga kujadili mikakati mbalimbali ya kuongeza idadi ya watu kukata bima kwa ajili ya mali zao.

Alisema kuwa katika operesheni hiyo wanayopanga kufanya, watashirikiana na Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) na itahusisha ukaguzi wa vyombo vya moto na vituo vya mafuta.

"Kwa kushirikiana Jeshi la Polisi na EWURA, tutafanya ukaguzi wa magari ambayo yako barabarani bila ya kuwa na bima na kuwakatia bima lakini pia tutakagua vituo vya mafuta ambavyo havina bima kama sheria inavyovitaka kuwa na bima ya majanga," alisema.

Shangali alisema pamoja na kufanya operesheni hiyo, pia wameweka mkakati wa kutoa elimu kwa wananchi kuhusu umuhimu wa kuwa na bima za mali na majanga mbalimbali.

"Watu wengi hawana bima za mali zao.

Hivi sasa kumekuwapo na matukio mengi ya nyumba kuungua moto, lakini nyumba nyingi hazina bima, hivyo tunapanga kutoa elimu kwa wananchi kuhusu umuhimu wa mali zao kukatiwa bima, ili kupata fidia pale majanga yanapotokea," alisema.

Aliwataka watoa huduma za bima hao kutumia vyombo vya habari kutoa elimu ya umuhimu wa bima kwa wananchi, ili kuongeza uelewa kwa jamii.

Mmoja wa watoa huduma kutoka Kampuni ya Jubilee Insurance, Irene Mbasha, alisema kama mikakati waliyojiwekea itatekelezwa, itakuwa na tija na kuongeza matumizi ya bima kwa Watanzania.



# Awataka wafanyabiashara kuchangamkia fursa kiwanda cha nondo, saruji Njombe

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

WAFANYABIASHARA wa Halmashauri ya Mji wa Makambako, wilayani Njombe, wametakiwa kutumia fursa ya kuwapo kiwanda cha kuzalisha nondo, saruji na kuunda magari kinachojengwa kijiji cha Ikelu, kwa kujenga nyumba na hoteli za kisasa, ili wanufaike kiuchumi.

Wito huo ulitolewa mwishoni mwa wiki na mchambuzi wa masuala ya kiuchumi na kisiasa mkoani Njombe, Oraph Mhema wakati akizungumza na waandishi wa habari mjini Makambako.

Alisema kutokana na ujenzi wa kiwanda hicho, wafanyabiashara wanatakiwa kuwekeza katika ujenzi wa hoteli za kisasa, kwa kuwa kiwanda hicho kitasababisha mwingiliano wa watu ambao ni lazima watahitaji huduma ya chakula na malazi.

Mhema alisema kuwa mbali na fursa hiyo kwa wafanyabiashara, serikali pia inatakiwa kujenga chuo cha ufundi mjini Makambako, ili kuzalisha wataalamu ambao watafanya kazi katika kiwanda hicho badala ya kuajiri watu kutoka nje ya mkoa huo.

“Makambako kwa sasa ninaiona mbali sana, serikali sasa itumie fursa hii kuleta vyuo vya ufundi, ili tusibaki nyuma kwenye mpango huu wa viwanda kwa sababu kama hatuna taaluma yoyote, tutabaki nyuma na watakuja wageni watachukua fursa zetu,” alisema Mhema.

> **“Makambako kwa sasa ninaiona mbali sana, serikali sasa itumie fursa hii kuleta vyuo vya ufundi, ili tusibaki nyuma kwenye mpango huu wa viwanda kwa sababu kama hatuna taaluma yoyote, tutabaki nyuma...**

Baadhi ya wananchi mjini Makambako, akiwamo Zawadi Chusi, walisema kujengwa kiwanda hicho kutakuza uchumi wao kutokana na kuongezeka mwingiliano wa watu pamoja na vijana wengi kupata ajira.

“Kwa ujenzi wa kiwanda hiki ni faida kwetu sisi Makambako, kwa sababu sisi wanawake tupo tunazunguka kuuza matunda, uji.

Kwahiyo, ujio wa hiki kiwanda utatusaidia sana kuinua uchumi wetu na kutusaidia kupeleka watoto shuleni,” alisema Zawadi.

Oktoba 10, mwaka huu, Balozi wa China nchini, Chen Mingjian, alitembelea eneo ambalo kiwanda cha kuzalinda nondo, saruji na kuunda magari kinachojengwa katika kijiji cha Ikelu na kampuni ya Fujian Hexingwang Industry.

Kiwanda hicho kinatarajiwa kuzalisha ajira za moja kwa moja kwa zaidi ya watu 500.



Waziri wa Nchi Ofisi ya wWaziri Mkuu (Sera Bunge na Uratibu), William Lukuvi (kushoto) ambaye ni Mbunge wa Isimani. mkoani Iringa, akizungumza na vijana baada ya kukabidhi mitungi ya gesi ikiwa ni jitihada za kumuunga mkono. Rais Samia Suluhu Hassan katika matumizi ya nishati safi ya kupikia. **PICHA: MPIGA PICHA WETU**

## Ridhiwani awaongoza wauguzi kupokea majiko, mitungi ya gesi

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu - Kazi, Vijana, Ajira na Watu Wenye Ulemavu, Ridhiwani Kikwete ameongoza zaidi ya wauguzi 200 katika Halmashauri ya Chalinze, mkoani Pwani kupokea msaada wa mitungi ya gesi na majiko.

Wauguzi hao ni wanaowahudumia kinamama wenye watoto njiti, mitungi hiyo ilitolewa na kampuni ya Oryx kwa kushirikiana na Doris Mollel Foundation.

Akizungumza wakati wa hafla hiyo iliyofanyika katika Hospitali ya Msoga, Ridhiwani alisema msaada huo ni sehemu ya kumuunga mkono Rais Samia Suluhu Hassan kuhusu kampeni ya matumizi ya nishati safi ya kupikia.

Alisema: “Wauguzi wetu kupatiwa mitungi hii ya gesi ni moja ya faida ambayo inakwenda kupatikana, sasa watakuwa na muda wa kutosha kuhudumia kinamama wenye watoto njiti katika hospitali yetu, kuni na mkaa vinasababisha muda mwingi kupotea.”

Alisema mkaa uliokuwa unapelekwa Dar es Salaam katika kipindi cha miaka mitatu hadi minne iliyopita, kwa zaidi ya asilimia 88 unatoka Chalinze.

Ridhiwani alisema hali hiyo iliwalazimu Chalinze kufanya operesheni maalumu ya kuangalia ndani ya Hifadhi ya Wamimbiki, hali ilivyo na kubaini sehemu kubwa imekuwa jangwa.

Muuguzi Mkuu wa Halmashauri ya Chalinze, Gabdiela Mtwale alisema watahakikisha wanawahamasisha wauguzi kutumia nishati safi kwa kuwa hata Rais Samia anahimiza wananchi kutumia nishati safi.

Mwakilishi wa Kampuni ya Oryx Gas Tanzania, Evarist Kisaka alisema: “Tunajua matumizi ya kuni na mkaa yanapoteza muda mwingi. Kuwapatia mitungi hii tunalenga kulinda afya za wauguzi wetu ili waendelee kuwahudumia vizuri kinamama wenye watoto njiti, pia tunahakikisha tunalinda mazingira kwa ujumla.”

Alisema gunia la mkaa la Sh. 80,000, kwa familia ya watu watatu linatumika muda wa mwezi mmoja kulinganisha na matumizi ya gesi ambayo gharama ni chini ya Sh. 60,000.

Msimamizi wa miradi kutoka Dorris Mollel Foundation, Alice Mwakatika alisema: “Tumewapa mitungi wauguzi hawa kwa sababu tunajua wanakuwa na muda mwingi na wagonjwa hasa kinamama. Sisi tumejikita katika afya ya uzazi (mama na mtoto)”.

# Watano washikiliwa polisi tuhuma za uhalifu

**Na Elizabet John,** NJOMBE

JESHI la Polisi Mkoa wa Njombe linawashikilia watu watano kwa tuhuma za makosa mbalimbali. Hao ni pamoja na Rogers Vegule (29) na Richard Joseph (31), wakazi wa kijiji cha Luduga, wilaya ya Wanging'ombe wanaotuhumiwa kwa uvunjaji na kufanya uharibifu katika Kanisa Katoliki wilayani humo.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Njombe, Kamishna Msaidizi Mahamoud Banga aliyasema hayo mwishoni mwa wiki na wakati akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake.

Kamanda Banga alisema watuhumiwa hao pia wanadaiwa kujihusisha na matukio mengine ya uvunjaji katika maeneo mengine ya Wanging'ombe, hivyo wanashikiliwa na watafikishwa mahakamani hivi karibuni.

Alisema kukamatwa kwa watuhumiwa hao kumetokana na operesheni mbalimbali na misako ambayo imefanyika katika kipindi cha mwezi Septemba mwaka huu.

Kamanda huyo alitaja tukio lingine kwamba, wanawashikilia Caspary Kayombo (64), Bernad Ndomba (44) na Bahati Gowele (49), wote wakazi wa kijiji cha Ngelenge, wilayani Ludewa kwa tuhuma za kukutwa na nyavu bandia ambazo wamekuwa wakizitumia kufanya uvuvi haramu.

Jeshi hilo pia linamshikilia Baraka Mtweve (61) kwa tuhuma za kukutwa na vipodozi ambavyo vimekatazwa na mamlaka husika, hivyo jeshi linafanya mawasiliano na mamlaka hiyo ili afikishwe mahakamani, pia kujua thamani ya vipodozi hivyo.

Joyce Ojala (32), mkazi wa Matalawe, Halmashauri ya Mji wa Njombe, anashikiliwa na jeshi hilo kwa tuhuma za kutoa taarifa za uongo kuwa ametekwa wakati kumbe haikuwa hivyo, bali alikuwa anasumbuliwa na wivu wa mapenzi.

Alisema mwanamke huyo alitoa taarifa kwa mume wake, Mfaume Mzee (37) kwamba ametekwa na watu wasiojulikana na anahitajika mumewe aende kwa sababu amekuwa akijihusisha na uhusiano na wake za watu.

“Kwa hiyo, hawa watu wamemteka ili mume aende mwenyewe lakini baada ya kutoa taarifa, Jeshi la Polisi wakati wa ufuatiliaji tulibaini kwamba huyu mama alikuwa amejiteka mwenyewe kwa wivu wa mapenzi,” alisema Kamanda Banga.

Alisema mume wa mtuhumiwa huyo alikuwa Songea, mkoani Ruvuma akifanya shughuli za madini na alikuwa hajarejea Njombe kwa muda mrefu, hivyo akaona atumie njia hiyo ili mumewe aweze kurejea.

Jeshi la polisi Mkoa wa Njombe limetoa wito kwa wananchi mkoani humo kutojihusisha na uhalifu pamoja na kutofumbia macho wahalifu, bali watoe taarifa mapema ili hatua stahiki zichukuliwe.



# Matukio 148 udhalilishaji yaripotiwa mwezi mmoja

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MATUKIO ya kesi 148 za udhalilishaji wa kijinsia visiwani Zanzibar, yameripotiwa katika maeneo mbalimbali Septemba, mwaka huu, huku ikionesha matukio hayo yamepungua kulinganishwa na Agosti uliokuwa na matukio 152.

Hayo yalisemwa na mwasilishaji kutoka Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali Zanzibar, Ahmada Hassan Suleimani, wakati akiwasilisha taarifa kwa waandishi wa habari kuhusu matukio ya udhalishaji visiwani humo.

Alisema wilaya ya Magharibi A Unguja inaongoza kwa kuwa na matukio 41, ikifuatwa na Magharibi B (37), wilaya ya Mjini (27), Chakechake Pemba (10) Micheweni na Wete kote matukio matatu.

Alisema kuwa Septemba, mwaka huu, matukio ya ulawiti yaliongezeka, kukiwa na matukio 64, ubakaji 15, kuingilia kinyume na maumbile sita, kutorosha tisa, shambulio 26 na shambulio la aibu 28.

Ofisa huyo alisema waathirika wa matukio hayo wengi ni wasichana ambao ni 62, wavulana 14, wanawake wawili na mwanamume mmoja.

Ahmada alisema kuwa bado kuna changamoto ya upatikanaji takwimu halisi hasa kwa matokeo hayo kutokana na baadhi ya familia za waathiriwa kumalizana katika ngazi za familia nyumbani.

Mkaguzi wa Polisi kutoka Makao Makuu ya Polisi Zanzibar, Makame Haji, alisema licha ya asasi za kiraia na taasisi za serikali kuendelea kutoa elimu katika jamii juu ya kuripoti matukio hayo katika vyombo vinavyohusika, baadhi ya jamii haifanyi hivyo na wazazi kuchangia ukatili wa kijinsia kushamiri katika jamii.

"Tunaona jitihada kubwa zinachukuliwa na taasisi za kiserikali, mashirika na hata hizi taasisi zisizo za serikali, lakini baadhi ya jamii hawajahamasika kuripoti haya matukio hasa kwa yale yanayafanywa ndani ya familia.

"Unakuta mzazi anaruhusu mtoto kuwa na uhuru mpana wa kufanya mambo na uamuzi pasipo kufikiri athari ya baadaye kwa mtoto huyo na pia kuwaamini watu juu ya mtoto hata kama ni ndugu, mume, mke na jamii unatakiwa uwaangalie kwa jicho la karibu katika kuhakikisha usalama wa watoto," alisema.

Katibu wa Baraza la Elimu na Mrajisi wa Elimu Zanzibar, Farid Ali Muhamad, alisema wanatoa elimu mbalimbali kwa waathirika wa matukio hayo ya udhalilisha, ili kuwajengea mazingira ya kuwa salama.

Aliwataka viongozi wa asasi za kirai kutosita kutoa ushirikiano, ili kuhakikisha jamii inajua athari mbalimbali za udhalilishaji na kuwalinda watoto kuingia katika vishawishi, ndoa za utotoni na mengineyo.

Meneja Program kutoka Shirika la Kimataifa la UN Women, Lucy Tesha, alisema wanaendelea kutoa elimu kwa jamii kuhusu udhalilishaji unaoendelea kila siku na kulitaka Jeshi la Polisi na viongozi wa dini kwa kushirikiana na taasisi nyingine, kuwa mstari wa mbele kufuatilia kwa kina suala la ukatili wa kijinsia katika jamii.




Bingwa wa Nyonga na Magoti kutoka hospitali ya Queen Elizabeth ya Uingereza, Prof. Mamoun Abdel Gadir (katikati), akipewa maua na Ofisa Utawala wa Global Medicare, Lucy Mendela (kulia), alipowasili nchini jana kwa ajili ya kufanya upasuaji wa nyonga na magoti kwa njia ya matundu madogo. Kushoto ni Meneja Mkuu wa Global Medicare, Daniel Lazaro. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# NMB yapewa tuzo maalumu kuwa benki ya kwanza duniani mfumo 'Lipa Kwa QR Link'

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

BENKI ya NMB imeendelea kuweka historia za mapinduzi katika utoaji huduma, baada ya kuwa benki ya kwanza duniani kuzindua Mfumo wa Malipo wa Lipa kwa QR Link (NMB QR Pay by Link), unaowawezesha wateja na wasio wateja wa benki hiyo kutoka kokote duniani, kufanya malipo kwa 'kuskani' QR za NMB kwa simu za mkononi.

Uzinduzi wa mfumo huo unaolenga kuongeza wigo wa malipo kwa wafanyabiashara walio nje ya mifumo rasmi ya malipo, zikiwamo Mashine za POS, ulifanyika Jumamosi, visiwani Zanzibar, mbele ya Mwakilishi Mkazi wa Mastercard Kanda ya Afrika Mashariki, Shehryar Bahk Ali.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ), Dk. Aboud Suleiman Jumbe, ni miongoni mwa mashuhuda wa uzinduzi wa mfumo huo na alishuhudia Mwakilishi huyo Mastercard akiikabidhi NMB tuzo maalumu, iliyopokewa na Ofisa Mkuu wa Wateja Binafsi na Biashara wa NMB, Filbert Mponzi.

Tuzo hiyo ni ya kutambua NMB kama benki ya kwanza duniani kuja na suluhusho hilo muhimu litakalosukuma mbele gurudumu la uchumi na maendeleo ya taifa kupitia sekta ya utalii Tanzania, Zanzibar na Tanzania Bara, ambapo kunakadiriwa kuwa na biashara ndogo milioni tatu zinazoajiri zaidi ya watu milioni tano.

Akizungumza wakati wa uzinduzi huo, Mponzi alisema NMB QR Pay by Link itawawezesha wateja wa kadi za benki yoyote duniani kufanya ununuzi au malipo kwenye huduma mbalimbali wakiwa nchini, ili mradi tu wawe na kadi za Mastercard, VISA na Union Pay.

"Wafanyabiashara wengi hapa Zanzibar wameshaanza kutumia huduma hii ya bure kulinganisha na mashine za POS ambazo ni ghali, na hiyo imetupa nguvu ya kuizindua, tukiamini kuwa suluhisho hili jipya linakwenda kusaidia ustawi wa maelfu ya Wazanzibari na Watanzania kwa ujumla.

"Mfumo huu ni rahisi, nafuu na salama, unaowaondolea changamoto mbalimbali watoa huduma, wakiwamo wenye hoteli, kampuni za watalii, maduka, kumbi za starehe, migahawa, wajasiriamali wa Forodhani, madereva teksi, wauzaji bidhaa za asili na vinyago, waendesha boti na wamiliki wa bodaboda.

"Ni mfumo wenye manufaa makubwa katika kukuza sekta ya utalii Tanzania, kupokea malipo kwa haraka, urahisi na unafuu kupitia kadi yoyote, zaidi ni fedha kuingia moja kwa moja katika akaunti na kuwezesha taarifa za kifedha za mwenye akaunti kutambulika kitaasisi na kuongeza vigezo vya kukopesheka," alisema Mponzi.

> **"Wafanyabiashara wengi hapa Zanzibar wameshaanza kutumia huduma hii ya bure kulinganisha na mashine za POS ambazo ni ghali, na hiyo imetupa nguvu ya kuizindua...**

Alishukuru serikali kupitia Benki Kuu ya Tanzania (BoT), kwa kuweka sera rafiki na mazingira bora na wezeshi ya utoaji huduma za kifedha na kwamba wanatambua na kuthamini juhudi za Serikali ya Awamu ya Nane ya SMZ na ya Awamu ya Sita ya Jamhuri ya Muungano, kama wadau wajibu wao ni kuwaunga mkono.

Bahk Ali aliitaja NMB kama kinara wa ubunifu wa kidigiti nchini na kwamba wao Mastercard wanatambua na kuthamini umahiri katika ubunifu unaofanywa na benki hiyo, kiasi cha kuweka rekodi hiyo ya kuzindua QR Pay by Link, hivyo kukabidhi tuzo maalumu.

Alifafanua kuwa kwa miaka mingi NMB imekuwa kinara wa mapinduzi ya kimfumo na kidigitali na kwamba Mastercard yenye kadi takribani milioni tano sokoni nchini, inajisikia fahari kwa ushirikiano wao, wakijivunia kila aina ya ubunifu, umahiri na huduma bora za taasisi hiyo.

"Tunaamini katika ubobezi wetu kwenye kuwezesha mifumo ya malipo, ndio maana hatusiti kupongeza ubunifu wa NMB uliozaa QR Pay by Link, mfumo unaokwenda kumaliza upotevu wa muda na kuwaepusha wajasiriamali, wafanyabiashara, kampuni na hata viwanda na gharama za kununua POS zinazofikia kiasi cha dola 300.

"Kwetu sisi Mastercard, tunaitazama NMB kama mshirika wa aina yake, kinara halisi wa huduma bora na mafanikio kwa nchi za Afrika Mashariki na Kati, ikiwagusa mamilioni ya wajasiriamali, mafanikio yote yakichagizwa na maono makubwa aliyonayo Ofisa Mtendaji Mkuu wake, Ruth Zaipuna," alisema Bahk Ali.

Kwa niaba ya Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale Zanzibar, Mudrick Ramadhani Soraga, Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Aboud Suleiman Jumbe, alipongeza NMB na Mastercard kwa ujio wa mfumo huo, unaokwenda kuleta mapinduzi ya kiuchumi, usimamizi, utoaji huduma na kutanua wigo wa vivutio vya utalii.

"Kama ilivyosemwa, soko la utalii Tanzania kwa mwaka huu kufikia Agosti, lilikwishaingiza watalii wa kimataifa zaidi ya milioni mbili, walioliingizia taifa takribani fedha za kigeni zinazokadiriwa kufikia dola bilioni 3.5, hao ni wa kimataifa katika nchi yenye watu za milioni 60, ambao ndani yake wamo watalii wa ndani," alisema.

# TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**FORM NO. A/1**
**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**JUDICIARY**
**IN THE HIGH COURT OF SONGEA**
**AT SONGEA**
**CIVIL CASE NO 16285 OF 2024**
**REGINA ELITERIUS NDONDE............PLAINTIFF(S)**
**VERSUS**
**NGAHOKOLA VILLAGE AND OTHERS................DEFENDANT(S)**
**SUMMONS TO FILE WRITTEN STATEMENT OF DEFENCE**
**(O.V.r 1 Civil Procedure Code)**
**TO: ADORAT NDUNGURU**

WHEREAS the above named Plaintiff(s) has/have instituted a suit against you upon the claim the particulars of which are set out in annexed copy of the plaint;
YOU ARE HEREBY NOTIFIED that you must file your WRITTEN STATEMENT OF DEFENCE in duplicate within twenty one (21) days of service of this notice upon you. If there is more than one plaintiff, additional copies of your written statement of defence must be filed sufficient for service on each of the Plaintiffs. If there are more defendants than one and the defence is not joint defence, there must be filed sufficient copies for service on each of the other defendants.
AND TAKE NOTICE that if you default in filing of the written statements of defence within the time specified the court may pronounce judgment against you.
TAKE FURTHER NOTICE that the case also has been fixed for order before Hon. E.L KAWISHE Judge/Magistrate on the 23 day of 10, 2024 at 9:00 O'clock in the forenoon/afternoon.
GIVEN UNDER MY HAND AND THE SEAL OF THE COURT this 14 day of 8, 2024.

REGISTRAR/MAGISTRATE

**FORM NO. A/1**
**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**JUDICIARY**
**IN THE HIGH COURT OF SONGEA**
**AT SONGEA**
**CIVIL CASE NO 16285 OF 2024**
**REGINA ELITERIUS NDONDE............PLAINTIFF(S)**
**VERSUS**
**NGAHOKOLA VILLAGE AND OTHERS................DEFENDANT(S)**
**SUMMONS TO FILE WRITTEN STATEMENT OF DEFENCE**
**(O.V.r 1 Civil Procedure Code)**
**TO: THOMAS MAPUNDA**

WHEREAS the above named Plaintiff(s) has/have instituted a suit against you upon the claim the particulars of which are set out in annexed copy of the plaint;
YOU ARE HEREBY NOTIFIED that you must file your WRITTEN STATEMENT OF DEFENCE in duplicate within twenty one (21) days of service of this notice upon you. If there is more than one plaintiff, additional copies of your written statement of defence must be filed sufficient for service on each of the Plaintiffs. If there are more defendants than one and the defence is not joint defence, there must be filed sufficient copies for service on each of the other defendants.
AND TAKE NOTICE that if you default in filing of the written statements of defence within the time specified the court may pronounce judgment against you.
TAKE FURTHER NOTICE that the case also has been fixed for order before Hon. E.L KAWISHE Judge/Magistrate on the 23 day of 10, 2024 at 9:00 O'clock in the forenoon/afternoon.
GIVEN UNDER MY HAND AND THE SEAL OF THE COURT this 14 day of 8, 2024.

REGISTRAR/MAGISTRATE

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA**
**WILAYA YA KINONDONI**
**MWANANYAMALA**
**SHAURI LA MADAI NAMBARI 434 LA 2021**
**SARA ELIFRIDA ARON**
**MWAMBU..............MUOMBAJI/WAOMBAJI**
**DHIDI YA**

- **MAISABO MBULIGI**
- **EMASHI GENERAL BROKERS LTD**
- **MEK ADVOCATES & LEGAL CONSULTANT......MDAIWA/WADAIWA**

**WITO KUITWA SHAURINI**

- **MAISABO MBULIGI**
- **EMASHI GENERAL BROKERS LTD**
- **MEK ADVOCATES & LEGAL CONSULTANT**

**POPOTE ULIPO/MLIPO**

SARA ELIFRIDA MWAMBU amefungua shauri mbele ya Baraza la Ardhi na Nyumba lililopo Kinondoni (Mwananyamala). Shauri husika limepangwa kutajwa/kusikilizwa tarehe 4/11/2024 saa 03:00 asubuhi/mchana mbele ya Mh. J.W. SILLAS. Hivyo unaamriwa kuhudhuria mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa.
Imetolewa na kutiwa Saini na Mhuri wa Baraza hili leo tarehe 05 Mwezi 08, 2024.

MWENYEKITI

**FORM NO. A/1**
**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**JUDICIARY**
**IN THE HIGH COURT OF SONGEA**
**AT SONGEA**
**CIVIL CASE NO 16285 OF 2024**
**REGINA ELITERIUS NDONDE............PLAINTIFF(S)**
**VERSUS**
**NGAHOKOLA VILLAGE AND OTHERS................DEFENDANT(S)**
**SUMMONS TO FILE WRITTEN STATEMENT OF DEFENCE**
**(O.V.r 1 Civil Procedure Code)**
**TO: TEODOLI MBAWALA**

WHEREAS the above named Plaintiff(s) has/have instituted a suit against you upon the claim the particulars of which are set out in annexed copy of the plaint;
YOU ARE HEREBY NOTIFIED that you must file your WRITTEN STATEMENT OF DEFENCE in duplicate within twenty one (21) days of service of this notice upon you. If there is more than one plaintiff, additional copies of your written statement of defence must be filed sufficient for service on each of the Plaintiffs. If there are more defendants than one and the defence is not joint defence, there must be filed sufficient copies for service on each of the other defendants.
AND TAKE NOTICE that if you default in filing of the written statements of defence within the time specified the court may pronounce judgment against you.
TAKE FURTHER NOTICE that the case also has been fixed for order before Hon. E.L KAWISHE Judge/Magistrate on the 23 day of 10, 2024 at 9:00 O'clock in the forenoon/afternoon

REGISTRAR/MAGISTRATE

**FORM NO. A/1**
**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**JUDICIARY**
**IN THE HIGH COURT OF SONGEA**
**AT SONGEA**
**CIVIL CASE NO 16285 OF 2024**
**REGINA ELITERIUS NDONDE............PLAINTIFF(S)**
**VERSUS**
**NGAHOKOLA VILLAGE AND OTHERS................DEFENDANT(S)**
**SUMMONS TO FILE WRITTEN STATEMENT OF DEFENCE**
**(O.V.r 1 Civil Procedure Code)**
**TO: SAILOS SON**

WHEREAS the above named Plaintiff(s) has/have instituted a suit against you upon the claim the particulars of which are set out in annexed copy of the plaint;
YOU ARE HEREBY NOTIFIED that you must file your WRITTEN STATEMENT OF DEFENCE in duplicate within twenty one (21) days of service of this notice upon you. If there is more than one plaintiff, additional copies of your written statement of defence must be filed sufficient for service on each of the Plaintiffs. If there are more defendants than one and the defence is not joint defence, there must be filed sufficient copies for service on each of the other defendants.
AND TAKE NOTICE that if you default in filing of the written statements of defence within the time specified the court may pronounce judgment against you.
TAKE FURTHER NOTICE that the case also has been fixed for order before Hon. E.L KAWISHE Judge/Magistrate on the 23 day of 10, 2024 at 9:00 O'clock in the forenoon/afternoon.
GIVEN UNDER MY HAND AND THE SEAL OF THE COURT this 14 day of 8, 2024.

REGISTRAR/MAGISTRATE

**FORM NO. A/1**
**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**JUDICIARY**
**IN THE HIGH COURT OF SONGEA**
**AT SONGEA**
**CIVIL CASE NO 16285 OF 2024**
**REGINA ELITERIUS NDONDE............PLAINTIFF(S)**
**VERSUS**
**NGAHOKOLA VILLAGE AND OTHERS................DEFENDANT(S)**
**SUMMONS TO FILE WRITTEN STATEMENT OF DEFENCE**
**(O.V.r 1 Civil Procedure Code)**
**TO: GODFREY MAPUNDA**

WHEREAS the above named Plaintiff(s) has/have instituted a suit against you upon the claim the particulars of which are set out in annexed copy of the plaint;
YOU ARE HEREBY NOTIFIED that you must file your WRITTEN STATEMENT OF DEFENCE in duplicate within twenty one (21) days of service of this notice upon you. If there is more than one plaintiff, additional copies of your written statement of defence must be filed sufficient for service on each of the Plaintiffs. If there are more defendants than one and the defence is not joint defence, there must be filed sufficient copies for service on each of the other defendants.
AND TAKE NOTICE that if you default in filing of the written statements of defence within the time specified the court may pronounce judgment against you.
TAKE FURTHER NOTICE that the case also has been fixed for order before Hon. E.L KAWISHE Judge/Magistrate on the 23 day of 10, 2024 at 9:00 O'clock in the forenoon/afternoon.
GIVEN UNDER MY HAND AND THE SEAL OF THE COURT this 14 day of 8, 2024.

REGISTRAR/MAGISTRATE

**FORM NO. A/1**
**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**JUDICIARY**
**IN THE HIGH COURT OF SONGEA**
**AT SONGEA**
**CIVIL CASE NO 16285 OF 2024**
**REGINA ELITERIUS NDONDE............PLAINTIFF(S)**
**VERSUS**
**NGAHOKOLA VILLAGE AND OTHERS................DEFENDANT(S)**
**SUMMONS TO FILE WRITTEN STATEMENT OF DEFENCE**
**(O.V.r 1 Civil Procedure Code)**
**TO: JANUARY MAPUNDA**

WHEREAS the above named Plaintiff(s) has/have instituted a suit against you upon the claim the particulars of which are set out in annexed copy of the plaint;
YOU ARE HEREBY NOTIFIED that you must file your WRITTEN STATEMENT OF DEFENCE in duplicate within twenty one (21) days of service of this notice upon you. If there is more than one plaintiff, additional copies of your written statement of defence must be filed sufficient for service on each of the Plaintiffs. If there are more defendants than one and the defence is not joint defence, there must be filed sufficient copies for service on each of the other defendants.
AND TAKE NOTICE that if you default in filing of the written statements of defence within the time specified the court may pronounce judgment against you.
TAKE FURTHER NOTICE that the case also has been fixed for order before Hon. E.L KAWISHE Judge/Magistrate on the 23 day of 10, 2024 at 9:00 O'clock in the forenoon/afternoon.
GIVEN UNDER MY HAND AND THE SEAL OF THE COURT this 14 day of 8, 2024.

REGISTRAR/MAGISTRATE

**FORM NO. A/1**
**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**JUDICIARY**
**IN THE HIGH COURT OF SONGEA**
**AT SONGEA**
**CIVIL CASE NO 16285 OF 2024**
**REGINA ELITERIUS NDONDE............PLAINTIFF(S)**
**VERSUS**
**NGAHOKOLA VILLAGE AND OTHERS................DEFENDANT(S)**
**SUMMONS TO FILE WRITTEN STATEMENT OF DEFENCE**
**(O.V.r 1 Civil Procedure Code)**
**TO: EVANGERISTA HAULE**

WHEREAS the above named Plaintiff(s) has/have instituted a suit against you upon the claim the particulars of which are set out in annexed copy of the plaint;
YOU ARE HEREBY NOTIFIED that you must file your WRITTEN STATEMENT OF DEFENCE in duplicate within twenty one (21) days of service of this notice upon you. If there is more than one plaintiff, additional copies of your written statement of defence must be filed sufficient for service on each of the Plaintiffs. If there are more defendants than one and the defence is not joint defence, there must be filed sufficient copies for service on each of the other defendants.
AND TAKE NOTICE that if you default in filing of the written statements of defence within the time specified the court may pronounce judgment against you.
TAKE FURTHER NOTICE that the case also has been fixed for order before Hon. E.L KAWISHE Judge/Magistrate on the 23 day of 10, 2024 at 9:00 O'clock in the forenoon/afternoon.
GIVEN UNDER MY HAND AND THE SEAL OF THE COURT this 14 day of 8, 2024.

REGISTRAR/MAGISTRATE

**FORM NO. A/1**
**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**JUDICIARY**
**IN THE HIGH COURT OF SONGEA**
**AT SONGEA**
**CIVIL CASE NO 16285 OF 2024**
**REGINA ELITERIUS NDONDE............PLAINTIFF(S)**
**VERSUS**
**NGAHOKOLA VILLAGE AND OTHERS................DEFENDANT(S)**
**SUMMONS TO FILE WRITTEN STATEMENT OF DEFENCE**
**(O.V.r 1 Civil Procedure Code)**
**TO: EVANGERISTA HAULE**

WHEREAS the above named Plaintiff(s) has/have instituted a suit against you upon the claim the particulars of which are set out in annexed copy of the plaint;
YOU ARE HEREBY NOTIFIED that you must file your WRITTEN STATEMENT OF DEFENCE in duplicate within twenty one (21) days of service of this notice upon you. If there is more than one plaintiff, additional copies of your written statement of defence must be filed sufficient for service on each of the Plaintiffs. If there are more defendants than one and the defence is not joint defence, there must be filed sufficient copies for service on each of the other defendants.
AND TAKE NOTICE that if you default in filing of the written statements of defence within the time specified the court may pronounce judgment against you.
TAKE FURTHER NOTICE that the case also has been fixed for order before Hon. E.L KAWISHE Judge/Magistrate on the 23 day of 10, 2024 at 9:00 O'clock in the forenoon/afternoon.
GIVEN UNDER MY HAND AND THE SEAL OF THE COURT this 14 day of 8, 2024.

REGISTRAR/MAGISTRATE

**FORM NO. A/1**
**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**JUDICIARY**
**IN THE HIGH COURT OF SONGEA**
**AT SONGEA**
**CIVIL CASE NO 16285 OF 2024**
**REGINA ELITERIUS NDONDE............PLAINTIFF(S)**
**VERSUS**
**NGAHOKOLA VILLAGE AND OTHERS................DEFENDANT(S)**
**SUMMONS TO FILE WRITTEN STATEMENT OF DEFENCE**
**(O.V.r 1 Civil Procedure Code)**
**TO: RUFINA L. NYANGU**

WHEREAS the above named Plaintiff(s) has/have instituted a suit against you upon the claim the particulars of which are set out in annexed copy of the plaint;
YOU ARE HEREBY NOTIFIED that you must file your WRITTEN STATEMENT OF DEFENCE in duplicate within twenty one (21) days of service of this notice upon you. If there is more than one plaintiff, additional copies of your written statement of defence must be filed sufficient for service on each of the Plaintiffs. If there are more defendants than one and the defence is not joint defence, there must be filed sufficient copies for service on each of the other defendants.
AND TAKE NOTICE that if you default in filing of the written statements of defence within the time specified the court may pronounce judgment against you.
TAKE FURTHER NOTICE that the case also has been fixed for order before Hon. E.L KAWISHE Judge/Magistrate on the 23 day of 10, 2024 at 9:00 O'clock in the forenoon/afternoon.
GIVEN UNDER MY HAND AND THE SEAL OF THE COURT this 14 day of 8, 2024.

REGISTRAR/MAGISTRATE

**FORM NO. A/1**
**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**JUDICIARY**
**IN THE HIGH COURT OF SONGEA**
**AT SONGEA**
**CIVIL CASE NO 16285 OF 2024**
**REGINA ELITERIUS NDONDE............PLAINTIFF(S)**
**VERSUS**
**NGAHOKOLA VILLAGE AND OTHERS................DEFENDANT(S)**
**SUMMONS TO FILE WRITTEN STATEMENT OF DEFENCE**
**(O.V.r 1 Civil Procedure Code)**
**TO: JOHN MBENDO**

WHEREAS the above named Plaintiff(s) has/have instituted a suit against you upon the claim the particulars of which are set out in annexed copy of the plaint;
YOU ARE HEREBY NOTIFIED that you must file your WRITTEN STATEMENT OF DEFENCE in duplicate within twenty one (21) days of service of this notice upon you. If there is more than one plaintiff, additional copies of your written statement of defence must be filed sufficient for service on each of the Plaintiffs. If there are more defendants than one and the defence is not joint defence, there must be filed sufficient copies for service on each of the other defendants.
AND TAKE NOTICE that if you default in filing of the written statements of defence within the time specified the court may pronounce judgment against you.
TAKE FURTHER NOTICE that the case also has been fixed for order before Hon. E.L KAWISHE Judge/Magistrate on the 23 day of 10, 2024 at 9:00 O'clock in the forenoon/afternoon.
GIVEN UNDER MY HAND AND THE SEAL OF THE COURT this 14 day of 8, 2024.

REGISTRAR/MAGISTRATE

**FORM NO. A/1**
**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**JUDICIARY**
**IN THE HIGH COURT OF SONGEA**
**AT SONGEA**
**CIVIL CASE NO 16285 OF 2024**
**REGINA ELITERIUS NDONDE............PLAINTIFF(S)**
**VERSUS**
**NGAHOKOLA VILLAGE AND OTHERS................DEFENDANT(S)**
**SUMMONS TO FILE WRITTEN STATEMENT OF DEFENCE**
**(O.V.r 1 Civil Procedure Code)**
**TO: MICHAEL KAYOMBO**

WHEREAS the above named Plaintiff(s) has/have instituted a suit against you upon the claim the particulars of which are set out in annexed copy of the plaint;
YOU ARE HEREBY NOTIFIED that you must file your WRITTEN STATEMENT OF DEFENCE in duplicate within twenty one (21) days of service of this notice upon you. If there is more than one plaintiff, additional copies of your written statement of defence must be filed sufficient for service on each of the Plaintiffs. If there are more defendants than one and the defence is not joint defence, there must be filed sufficient copies for service on each of the other defendants.
AND TAKE NOTICE that if you default in filing of the written statements of defence within the time specified the court may pronounce judgment against you.
TAKE FURTHER NOTICE that the case also has been fixed for order before Hon. E.L KAWISHE Judge/Magistrate on the 23 day of 10, 2024 at 9:00 O'clock in the forenoon/afternoon.
GIVEN UNDER MY HAND AND THE SEAL OF THE COURT this 14 day of 8, 2024.

REGISTRAR/MAGISTRATE

## KUPOTEA KWA CHETI



**AMANIELI KENEDY ALLI** anatangaza kupotea kwa Cheti cha Kidato cha nne yenye index namba S.48630048 kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **PARENI SECONDARY SCHOOL** mwaka **2013**. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **REF:MWA/MAG/376/2017.**

## TANGAZO LA NOTISI – KWA MDAIWA

**TUJIJENGE TANZANIA FINANCIAL SERVICES LIMITED**, Inatangaza notisi kwa mdhamini tajwa hapo chini aliyedhamini mkopo na kushindwa kulipwa kulingana na masharti na makubaliano ya mkataba wa mkopo
**BAKARI SALUM MAPANDE** wa Charambe Mtaa wa Mchikichini wilaya ya Temeke - Dar Es Salaam. Hii ni notisi ya siku Sitini (Siku 60) kutakiwa kulipa deni la mkopo kwa kumdhamini ndugu **CYRIL MICHAEL WARIRO**
Unatakiwa kulipa deni la mkopo mnalodaiwa na Tujijenge ndani ya muda husika ulioainishwa siku 60.
Hii ni baada ya mkopaji kushindwa kulipa kulingana na masharti na makubaliano ya mkataba.
Notisi hii itatumika kuanzia tarehe ya Tangazo hili gazetini. Hatua zaidi za Kisheria zitachukuliwa dhidi yako endapo kama utashindwa kulipa deni la mkopo ndani ya muda ulioainishwa/kutangazwa.
Ikiwa ni pamoja na kufuata taratibu nyingine za kisheria za kuruhusu dalali kuuza mali zilizotumika kudhamini mkopo uliochukuliwa.

**Kwa Mawasiliano piga:**
**+255 222774742-3/0718068335**
**Au Email: tujijengetanzania@tujijenge.or.tz**

## MNADA WA HADHARA

**SEPCO Debt Collections & Auctioneering Co. Ltd** tunatangazia umma kuwa kutakuwepo na mnada wa hadhara wa kuuza dhamana ya mdaiwa kama ilivyoonyeshwa kwenye jedwali hapo chini. Mnada utaendeshwa kwa idhini tuliyopewa na Tujijenge Tanzania Financial Services Ltd kama ilivyotangazwa gazetini:-

| Mdaiwa | Dhamana/ Mahali ilipo | Tarehe ya mnada | Dalali |
|---|---|---|---|
| Samwel Ezekiel Masunga | Gari T.977 EEN ToyotaHIACE -SEPCO Yard Tabata.30 | 30/10/2024 | SEPCO Debt Collections & Auctioneering Co. Ltd |

**Masharti Mengine:**
Mnada utafanyika mahali dhamana ilipo kuanzia saa nne asubuhi. Mteja atalipa 25% siku ya mnada, 75% atalipa ndani ya siku 14, akishindwa kulipa 25% iliyolipwa hairudishwi na mnada utarudiwa tena.

Gharama za kuona, kukagua, kuhamisha umiliki, kumtoa mdaiwa/mpangaji ni juu ya mnunuzi.

**Mawasiliano piga:**
**SEPCO: 0715683777/ 0716535221**
**Tujijenge (T) Financial Services Ltd: 0718068335**

**IN THE COURT OF DISTRICT DELEGATE OF MOROGORO**
**DISTRICT AT MOROGORO**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO.23599 OF 2024**
**In the Matter of the late**
**DAMAS BAHIMO KAVISHE**

**1. REGINA J KAVISHE**
**2.............................................**
ALL persons claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate(or letter of administration) is made to the above- named pepetitioner.
Objection to the grant should be filed on or before the 22 day of OCT,2024.
Dated at Morogoro this 01 day of OCT 2024.

RESIDENT MAGISTRATE

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO BOMA**
**WILAYA YA MOROGORO**
**MKOA WA MOROGORO**
**Usimamizi wa Mirathi Na...36/2024**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA**
**MAREHEMU: SAIDY HASSAN BUSHIRY wa K/NDEGE**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI**
**YALIYOLETWA NA BUSHIRY SAIDY HASSAN**
**TANGAZO**
**(kanuni ya 5 (2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo Tarehe 25 Mwezi 10 Mwaka 2024 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
Zingatia;

- Endapo kuna yoyote mwenye wosia wa marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
- Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani na waweza kukaguliwa
- Marehemu hakuacha wosia

Imetolewa leo Tarehe 04 mwezi 10 mwaka 2024

.........
**HAKIMU**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakana ya Mwanzo KAWE Wilaya ya KINONDONI**
**Kituo cha KAWE Mkoa wa DAR ES SALAAM**
**Shauri la Madai No: 449/ 2024**
**Jina la Mdai: L.K MICROFINANCE (KELVIN LIBENEKA)**
**Jina la Mdaiwa: ANNA IVAN SUTILA (MBEZI JUU DAR ES SALAAM)**
**Kwa kuwa Mdai/Wadai ameleta/wameleta madai yake/yao kwamba (Eleza hapa habari za madai)**

**KUJIBU MADAI YA PESA TSH. 1,162,000**
kwa hivyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika mahakama hii tarehe 28 Mwezi 10 Mwaka 2024 Saa 2:30 Asubuhi/Mchana kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea .

**ANGALIZO:** kama hautahudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila ya wewe kuwepo
Hati hii imetolewa Kwa Amri na Muhuri wa Mahakama leo hii tarehe 17 mwezi 10 mwaka 2024

HAKIMU MKAZI
MAHAKAMA YA MWANZO
KAWE

**IN THE HIGH COURT OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**ARUSHA SUB REGISTRY**
**(LABOUR DIVISION)**
**AT ARUSHA**
**REVISION NO 37 OF 2023**

**(Originating: CMA/ARS/ARS/227/22/115/22)**

**NOTICE OF MENTION**
**SALIM MOHAMED MANONGA...........APPLLICANT**
**VERSUS**
**JAMBO FOOD PRODUCT LIMITED..........RESPONDENT**

**TO: JAMBO FOOD PRODUCT LIMITED**

**TAKE NOTICE** that the above case has been fixed for Mention in the high court at Arusha on the **23th Day of October 2024** at 9:00 o'clock in the forenoon, before **Hon. D.D. Ndumbaro, Judge.**

You may appear in person or by advocate or agent duly authorized to appear on your behalf and you are directed to produce on that day all documents upon which you intend to rely in support of your case.

**TAKE FURTHER NOTICE THAT** in default of you appearance on that day and time before Mention or hearing the court may proceed in your absence.

**GIVEN under my HAND** and the **SEAL** of the **COURT** this 14th day of Agust, 2024

DEPUTY REGISTRAR
HIGH COURT
ARUSHA

**Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku**
**Piga Simu 0677020701**

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# Watumishi wa Gachagua kwenda likizo ya lazima

**NAIROBI,** Kenya

MAMLAKA katika Ofisi ya Naibu Rais wa Kenya aliyeondolewa madarakani Rigathi Gachagua (pichani chini), imewaagiza maofisa 108 wa ngazi za juu katika ofisi hiyo, kwenda likizo ya lazima, wakiwamo baadhi ya washauri wakuu wa Naibu Rais huyo.

Katika taarifa iliyotolewa jana, ilibainisha kuwa utekelezaji wa agizo hilo ulianza juzi, Jumamosi, saa 6:00 mchana, ikielezwa kuwa katika barua ya ndani ya usimamizi, mamlaka hiyo pia imesitisha mikataba yote ya wafanyakazi wa kandarasi za muda.

"Maofisa wote walioorodheshwa katika vikundi vya kazi T na U wanaagizwa kwenda likizo ya lazima mara moja," ilisoma risala iliyoandikwa na Patrick Mwangi, Katibu Mkuu Tawala katika Ofisi ya Naibu Rais.

Risala hiyo ambayo pia nakala yake ilitumwa kwa mkuu wa utumishi wa umma wa ikulu, ilisema kuwa agizo hilo linatekelezeka kuanzia saa sita mchana, Jumamosi.

Hii inakuja wakati Rais William Ruto, anakabiliwa na changamoto nyingine ya kumteua atakayeshikilia wadhifa wa Naibu Rais, huku kesi za kupinga chaguo lake zikiwasilishwa mahakamani.

Wakati huo huo, Mahakama nchini humo iliagiza Ijumaa, kusitishwa utekelezwaji wa kumoundoa Gachagua kutoka ofisini pamoja na mchakato wa kumteua mrithi wake hadi Oktoba 24, mwaka huu, ambako kesi hiyo itaamuliwa mbele ya jopo la majaji watatu. **TRT**



# Wakili wa mgombea upinzani Msumbiji auawa

**MAPUTO,** Msumbiji

EVINO Dias, aliyekuwa wakili wa mgombea mkuu wa upinzani kwenye uchaguzi wa urais uliofanyika Oktoba 9, mwaka huu, Venancio Mondlane, ameuawa kwa kupigwa risasi mjini Maputo.

Wakili huyo, Evino Dias, aliuawa kwa shambulio la risasi jana, pamoja na mgombea mwingine, Paulo Guambe wa chama cha PODEMOS, kinachomuunga mkono Mondlane.

Mashahidi wa tukio hilo walisema watu wawili wenye silaha walilifyatulia risasi gari la wawili hao, lililokuwa limeegeshwa kwenye barabara katikati mwa mji huo mkuu.

Kiongozi wa chama cha



PODEMOS, Albino Forquilha, alithibitishia vifo hivyo kwa shirika la habari la AFP, huku chama cha mawakili nchini humo kikieleza kushtushwa na mauaji ya Dias.

Polisi ilisema uchunguzi umeanzishwa lakini haikuthibitisha mara moja utambulisho wa watu hao wawili waliouawa.

Umoja wa Ulaya (EU), umetoa taarifa ya kulaani mauaji ya Dias na Guambe na kutoa wito wa uchunguzi kamili na wa wazi utakaowawajibisha wale waliohusika na uhalifu huo.

Ilielezwa kuwa hayo yanajiri wakati nchi hiyo ikisubiri matokeo ya uchaguzi ambao umeshuhudiwa kuibua madai zaidi ya wizi wa kura na kubana upinzani, dhidi ya chama tawala kwa muda mrefu.

Aidha, wachambuzi wa masuala ya kisiasa walisema mauaji hayo ni ushahidi zaidi wa wazi wa ukosefu wa haki ambao wote wanakabiliwa nao.

PODEMOS ni chama kipya cha upinzani ambacho kilipinga utawala wa miaka 49 wa chama cha 'Front for the Liberation of Mozambique' (FRELIMO) katika uchaguzi wa Oktoba 9, mwaka huu.

Ingawa Mondlane aligombea urais kama mtu huru, aliungwa mkono na PODEMOS. Na kwamba wote waliungana na vyama vingine vya upinzani kuishutumu FRELIMO, kwa udanganyifu katika uchaguzi na kuvuruga uchaguzi.

Hata hivyo, ilielezwa kuwa mgombea wa FRELIMO, Daniel Chapo anashikilia uongozi wa wazi katika kinyang'anyiro cha urais, kutokana na matokeo ya awali.

Matokeo ya mwisho ya uchaguzi yanatarajiwa kutangazwa wiki ijayo na kwamba Chapo anatarajiwa kutangazwa mshindi na kurithi mikoba ya Rais Filipe Nyusi, ambaye amehudumu kwa mihula miwili. **TRT**



Waziri wa Mambo ya Nje wa Ukraine, Adrii Sybiha (kulia), akimkaribisha mwenzake wa Ufaransa, Jean-Noel Barrot, mjini Kiev juzi, baada ya taifa hilo kutoa msimamo wake wa kuiunga mkono Ukraine katika hatua za kumaliza vita ambavyo vimedumu kwa miaka miwili sasa. **PICHA: MTANDAO**

# Raia wa Uingereza, Uturuki watekwa nyara Kenya

**NAIROBI,** Kenya

RAIA wa Uingereza ameiambia BBC kuwa yeye na wenzake kadhaa wa Uturuki wametekwa nyara na watu waliojifunika nyuso zao nchini Kenya, licha ya kutobainisha sababu ya tukio hilo.

Akifafanua kuhusu mkasa huo jana, Necdet Seyitoğu, alisema tukio hilo lilifanyika siku ya Ijumaa, jijini Nairobi, na kwamba Waturuki wanne kwa sasa hawajulikani waliko.

Seyitoğu, ambaye aliishi nchini Uingereza kwa miaka 18 kabla ya kuhamia Kenya miaka miwili iliyopita, alisema aliachiwa baada ya saa nane alipowaonesha wanaodaiwa kumteka nyara nakala ya pasipoti yake ya Uingereza.

Katika taarifa, iliyotolewa na Ofisi ya Mambo ya Nje ya Uingereza, ilisema wanatoa usaidizi wa kibalozi kwa Mwingereza na familia yake baada ya tukio lililotokea nchini humo.

Akizungumzia tukio hilo, Msemaji wa Keshi la Polisi nchini Kenya, Resila Onyango, alisema watu wanane waliokuwa na silaha walitoka kwenye magari hayo mawili na kuwatoa watu wawili waliokuwa ndani na kuondoka nao.

Alisema baadaye, Yusuf Kar mmoja wa raia wa Uingereza mwenye asili ya Uturuki, aliripoti tukio hilo katika kituo cha polisi kilicho karibu na kuwataja watu waliotekwa nyara kuwa ni Hüseyin Yeğlsu na Necdet Seyitoğu.

Mamlaka ya Uturuki, bado haijazungumzia chochote kuhusiana na tukio hilo, ikielezwa kuwa kwa sasa liko katika hatua za uchunguzi unaofanywa na Mamlaka ya Upelelezi wa Makosa ya Jinai (DCI).

Tawi la Nairobi la Tume ya Umoja wa Mataifa ya Kuhudumia Wakimbizi pia limesema kwamba (UNHCR) imepokea taarifa juu ya tukio hilo na tutazidi kuutaarifu umma zaidi pindi tutakapozipata."

Hata hivyo, ilielezwa kuwa watu waliopotea walisemekana kuwa chini ya ulinzi wa Umoja wa Mataifa (UN), jijini Nairobi.

Hayo yanaendelea wakati taifa hilo likikabiliwa na masuala mbalimbali ya kisiasa, ikiwamo mchakato wa kumuondoa naibu rais wa nchi hiyo madarakani, mchakato ambao unatupiwa macho na wananchi wa ndani na hata nje ya mipaka ya Kenya. **BBC**

HABARI MICHEZO

# MAJERUHI WATAJWA SABABU TANZANIA KUPOTEZA BAFCON

Na Adam Fungamwango

KOCHA Mkuu wa Timu ya Taifa ya Tanzania ya Soka la Ufukweni, Jaruph Juma, amesema kipigo cha mabao 4-3 walichokipata dhidi ya Morocco juzi, kilitokana na baadhi ya wachezaji wake kupata majeraha na kutomaliza mchezo.

Akizungumza kutoka mjini Hurghada, Misri, kocha huyo alisema wangeweza kushinda mechi hiyo, lakini baadhi ya wachezaji wake walianza kuumia na kutoka kitu ambacho kiliwapa ahueni wapinzani wao.

**Alisema hayo baada ya kumalizika kwa mchezo huo wa kwanza wa michuano ya fainali za Mataifa ya Afrika kwa Soka la Ufukweni (BAFCON) 2024, zinazofanyika nchini humo, ikizishirikisha jumla ya timu nane Afrika.**

"Changamoto iliyojitokeza dakika za mwanzoni tulipoteza baadhi ya wachezaji wetu tegemeo ambao walipata majeraha, mchezo huu una wachezaji wachache tu uwanjani, unapoteza wachezaji watatu tegemeo ni mbaya sana," alisema kocha huyo ambaye pia alicheza mchezo huo na kufunga bao.

Akizumgumzia mchezo huo kwa ujumla, alisema ulikuwa mgumu kama alivyotabiri awali, lakini akawataka Watanzania wasikate tamaa kwani wana michezo mingine miwili imebaki.


"Tunashukuru mechi imeisha salama, ulikuwa mgumu kama nilivyotangulia kusema kabla, kwa sababu ulikuwa unaamua sura nzima ya mashindano, maandalizi yetu yalikuwa mazuri sana, matokeo hayakuwa mazuri kwetu.

Mchezo huu utakuwa chachu kwa inayofuata dhidi ya Misri na Ghana, tutafanya kila linalowezekana kushinda michezo itakayofuata dhidi ya Misri ambao ni wenyeji, natabiri utakuwa mgumu zaidi, lakini pia wachezaji wetu nadhani watakuwa wameshapona na wa mwisho ni dhidi ya Ghana," alisema.

Tanzania ipo Kundi A, ambapo mbali na Morocco, wapo wenyeji Misri na Ghana, huku Kundi B likiwa na timu za Senegal, Msumbiji, Malawi na Mauritania.

Ratiba inaonesha kuwa baada ya mchezo huo, Tanzania itarejea tena uwanjani leo, Oktoba 21, kucheza dhidi ya wenyeji Misri na Oktoba 22 itakutana na Ghana.

HII HAPA...!




Kiungo Mshambuliaji wa Simba, Kibu Denis, akiwekwa mtu kati na wachezaji wa Yanga, Chadrack Boka (kulia) na Khalid Aucho, katika mechi ya 'Derby ya Kariaoko' ya Ligi Kuu Bara iliyopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam juzi na Yanga kushinda bao 1-0. Katika harakati hizo za Kibu kutaka kuivuka ngome ya Yanga, Boka alimchezea rafu mbaya ndani ya 18, moja ya tukio kati ya mawili ambayo Mwamuzi Ramadhani Kayoko, analalamikiwa kwa kutotoa penalti kwa Simba. **MPIGAPICHA WETU**

## Mwembe Makumbi City yazitaka tatu za Mlandege leo

Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR

KOCHA wa timu ya Mwembe Makumbi City, Rajab Mrisho, amesema anawaheshimu Mlandege FC kwa kuwa ni wakongwe katika soka la Zanzibar na wana uzoefu katika Ligi Kuu, lakini amejiandaa kukabiliana nao vilivyo.

Mwembe Makumbi City itashuka uwanjani leo, Jumatatu kuwakabili Mlandege FC katika mchezo wa ligi hiyo, utakaopigwa majira ya saa kumi alasiri kwenye Uwanja wa New Amaan Complex, ikiwa ni mwendelezo wa Ligi Kuu Zanzibar inayodhaminiwa na Benki ya Watu wa Zanzibar, PBZ.

Akizungumza na gazeti hili kocha huyo alisema kikosi chake kimejiandaa kukabiliana na timu yoyote itakayokuja mbele yao hasa katika kusaka alama tatu muhimu.

Alisema anajua mchezo huo utakuwa mgumu kwa kuwa wapinzani wao watataka kupata alama tatu muhimu, mpango ambao unafanana na Mwembe Makumbi City.

## Pengo ajigamba pambano la SGR

Na Shufaa Lyimo

BONDIA Habibu Pengo wa Dar es Salaam, amejigamba vikali kumtwanga mpinzani wake, Ayubu Mwankina kutoka Morogoro katika pambano la Homa ya SGR litakalofanyika Ijumaa wiki hii kwenye Ukumbi wa Tanzanite mkoani Morogoro.

Akizungumza na Nipashe jana, bondia huyo alisema amejiandaa vizuri kumshushia kipigo mpinzani wake kwani anamfahamu vema.

"Nitahakikisha heshima yangu inarudi kwa kumshushia Ayubu kichapo ambacho hatakaa akisahau katika maisha yake yote," alisema Pengo.

Alisema kutokana na kiwango alichokuwa nacho hakuna bondia yoyote ambaye anaweza kumpiga kwa KO siku hiyo kutokana na maandalizi anayoyafanya.

Kwa upande wa Kocha Mkuu wa bondia huyo, Haji Ngoso, alisema hana wasiwasi na bondia wake kutokana na mazoezi anayompa.

# *Stand United wazinduka, wazindua jezi mpya*

Na Marco Maduhu, SHINYANGA

HUKU ikiwa tayari imecheza michezo mitano ya Ligi ya Championship na kujikusanyia pointi 10 zinazoiweka katika nafasi ya tano kwenye msimamo wa ligi hiyo, Stand United ndiyo kwanza wamezinduka na juzi kuzindua rasmi jezi zake mpya za msimu huu wa 2024/25.

Stand United ambayo ilianza msimu mpya na jezi za zamani katika michezo mitano iliyocheza hadi sasa, imeshinda mitatu, sare moja na kupoteza mmoja.

Akizungumzia uzinduzi huo, ambao ulifanyika juzi katika Uwanja wa Nguzo Nane Manispaa ya Shinyanga, Msemaji wa timu hiyo, Ramadhani Zoro, alisema jezi hizo mpya zinapatikana katika maduka mbalimbali kwa bei ya Sh.25,000 na zitatumika katika msimu wa Ligi ya Championship 2024/25.

Mwenyekiti wa Kamati ya Mashindano na Usajili wa timu hiyo, Chrispin Kakwaya, alisema jezi hizo mpya zina ubora wa hali ya juu, na kwamba Stand United hivyo waisapoti timu yao kwa kuzinunua.

Kwa upande wa Kocha Mkuu wa Stand United, Meja Abdul Mingange, akizungumza kwenye uzinduzi wa jezi hizo, aliwaomba mashabiki wa timu hiyo maarufu kama 'Chama la Wana', kujitokeza kwa wingi kuiunga mkono timu hiyo, ili aendelee kufanya vizuri katika mechi zake na hatimaye kupanda Ligi Kuu Tanzania Bara.

"Mchezo wa mpira wa miguu unahitaji kuungwa mkono, tunawaomba mashabiki wa timu ya Stand United wawe pamoja na timu yao muda wote," alisema Mingange.

Aidha, aliongeza mchezo ujao wataikaribisha timu ya Bigman na kuwaomba mashabiki kujitokeza kwa wingi uwanjani, ili wapate pointi tatu, kabla ya michezo miwili inayofuata dhidi ya Mbeya Kwanza na Biashara United, ambapo lengo lao ni kuvuna alama zote tisa kwenye mechi hizo tatu.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### KYLE WALKER KUUZWA

KLABU ya Manchester City, iko tayari kumuuza nahodha Kyle Walker, 34, kwa takriban pauni milioni 15 msimu ujao wa majira ya joto. Beki huyo wa England analengwa na Al-Ahli ya Saudi Arabia. ***(Daily Star)***

### BUONANOTTE AWANIWA

MANCHESTER City na Liverpool zimeonesha nia ya kumnunua fowadi wa Brighton Facundo Buonanotte, 19, ambaye yuko kwa mkopo Leicester City. ***(Fichajes)***

### KERKEZ BEI JUU

KLABU ya Bournemouth itataka "fedha nyingi" kama watamuuza beki wa Hungary, Milos Kerkez, 20, ambaye anazivutia Liverpool, Arsenal na Manchester United. ***(Football Insider)***

### SCHLOTTERBECK KUMRITHI DIJK

LIVERPOOL inamlenga beki wa Borussia Dortmund na Ujerumani, Nico Schlotterbeck, 24, kama mbadala wa Virgil van Dijk, iwapo Mholanzi huyo ataondoka katika klabu hiyo msimu ujao wa majira ya joto. ***(Caught Offside)***

### SEMENYO AITAKA ARSENAL

ARSENAL imetiwa moyo iwapo inataka kumnunua mshambuliaji wa Bournemouth, Antoine Semenyo, 24, baada ya kusema yeye ni shabiki wa 'Washikabunduki' hao na anataka kucheza soka ya Ligi ya Mabingwa Ulaya. ***(Football 365)***

### FERNANDEZ KURUDI UNITED

KLABU ya Manchester United huenda ikamsajili tena beki wa kushoto, Alvaro Fernandez , 21, ambaye alijiunga na Benfica kwa mkataba wa kudumu msimu wa majira ya joto na anafuatiliwa na Liverpool na Real Madrid. ***(Teamtalk)***

### BARCA NA NYOTA WAKE

BARCELONA imeanzisha mazungumzo ya mkataba kuhusu makubaliano mapya kwa mlinzi Ronald Araujo, 25, anayelengwa na Manchester United na Chelsea - na kiungo Frenkie de Jong, 27, ambaye pia anasakwa na Mashetani Wekundu. ***(90 min)***

### POGBA BASI TENA JUVENTUS

KIUNGO wa kati wa Ufaransa, Paul Pogba, 31, anaonekana kutokuwa na uwezekano wa kuichezea tena Juventus mara tu marufuku yake ya kutumia dawa za kusisimua misuli itakapokamilika Machi baada ya mkurugenzi wa klabu hiyo kusema kuwa kikosi kimekamilika bila yeye. ***(DAZN, via ESPN)***

### TUCHEL NA ENGLAND

KOCHA wa England, Thomas Tuchel, atapokea marupurupu ya pauni milioni tatu ikiwa anaweza kuiongoza England kushinda Kombe la Dunia la 2026. ***(The Sun)***

### GUEHI ATAKIWA NEWCASTLE

KLABU ya Newcastle United iko tayari kufufua mpango wa kumsajili beki wa England na Crystal Palace, Marc Guehi, 24 kwa takriban pauni milioni 80. ***(Team Talk)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# RICE ALIA NA WACHEZAJI WENZAKE ARSENAL IKIFA

**LONDON,** England

DECLAN Rice amewajia juu wachezaji wenzake wa Arsenal, baada ya kichapo cha mabao 2-0 kutoka kwa Bournemouth ambapo walimaliza mchezo wakiwa 10 kwa mara ya tatu msimu huu.

**Mchezo huo uliopigwa kwenye Uwanja wa Vitaly uligeuka kuwa mgumu kwa Arsenal baada dakika ya 30 William Saliba kutolewa nje kwa kadi nyekundu kwa kumchezea vibaya Evanilson.**

Mchezaji huyo wa Kimataifa wa Ufaransa, awali alioneshwa kadi ya njano kabla ya ukaguzi wa VAR kubadilisha na kuwa nyekundu.

> ●●● Tumejifunga mara tatu, hatuwezi kufanya makosa ya kipuuzi, unahitaji nyota wako...

Bournemouth walianza kucheza kwa juhudi kubwa zaidi za kushambulia na walipata bao dakika ya 70 lililofungwa na Ryan Christie, kabla ya mkwaju wa penalti wa Justin Kluivert kuiweka pabaya Arsenal na kujikuta wakipoteza kwa mara ya kwanza msimu huu.


"Tumejifunga mara tatu katika mechi nane nyumbani kwa Brighton na ugenini kwa Manchester City. Bournemouth wametufunga 2-0," alisema Rice akiiambia Sky Sports baada ya mchezo huo.

"Najivunia wachezaji kwa kupigana hata tulipobakia 10, lakini tunatakiwa kuacha kufanya makosa, kwa sababu tunatakiwa wachezaji 11 kwa dakika 90.

"Tukiwa na wachezaji 10 tulionesha tabia na haiba nyingi kusalia kwenye mchezo. Nafasi kubwa ilikuwa ya Gabriel Martinelli na kipa aliisoma na kuokoa.

"Hatuwezi kufanya makosa ya kipuuzi, unahitaji wachezaji wako wote bora uwanjani wakati wote. Imani ni kubwa na tutashikamana. Huu ni mpira wa miguu, chochote kitakachotokea cha muhimu ni kushikamana na kubaki pamoja."

# TEN HAG AJIFUTUA KUIFUNGA BRENTFORD



**MANCHESTER,** England

ERIK ten Hag, amekiri Manchester United ilirejea kwa moto katika kipindi cha pili dhidi ya Brentford, baada ya kukasirishwa na mazingira ya bao la kwanza la utata la wageni hao kwenye mchezo wa Ligi Kuu, juzi Jumamosi.

United ilihitaji mabao ya kipindi cha pili kutoka kwa Alejandro Garnacho na Rasmus Højlund, ili kutoka nyuma na kushinda 2-1 ushindi wao wa kwanza kwenye michezo sita katika mashindano yote.

United walikuwa na hasira ya kwenda mapumziko wakiwa nyuma kwa bao 1-0 baada ya Ethan Pinnock kwa mpira wa kona huku Matthijs de Ligt akiwa nje ya uwanja akipokea matibabu ya jeraha la kichwa.

Aidha, ilikuwa ni mara ya tatu kwa De Ligt aliyetokwa na damu kuamriwa kutoka nje ya uwanja na Brentford alichukua nafasi hiyo.

"Ilikuwa damu, hivyo alikuwa tayari ametibiwa jeraha hilo," alisema Ten Hag.

"Sikuelewa kwa nini alitolewa nje. Nilikwenda kwa Matthijs na akasema 'ni damu lazima nitoke, sijui kwa nini.' Ilikuwa wakati mzuri sana kwa sababu Brentford ni wazuri sana kwenye kona na unakosa moja ya vichwa vyako bora zaidi."

Msaidizi wa Ten Hag, Ruud van Nistelrooy, alioneshwa kadi ya njano kwa kurushiana maneno na Ofisa wa Nne, Gavin Ward, yaliendelea hadi mapumziko.

"Bila shaka, tulikuwa na hasira wakati wa mapumziko," alisema.

"Unaona umoja, ari ya mapigano na tunaongeza ari ya kufunga mabao. Takwimu zinaonesha tunacheza soka nzuri msimu huu na hatufungi vya kutosha, lakini leo (juzi), tumefunga mabao mawili maridadi."

Ushindi kwa United utapunguza shinikizo kwa Ten Hag kabla ya safari ya Alhamisi kuwakabili Fenerbahce ya Jose Mourinho.

# Neymar rasmi arejea dimbani




**RIYADH,** Saudi Arabia

NEYMAR atarejea kwenye kikosi cha Al Hilal, kwa ajili ya mechi yao ya Ligi ya Mabingwa Asia wiki ijayo, baada ya kukaa nje ya uwanja kwa mwaka mmoja kutokana na jeraha, klabu hiyo ya Saudi Arabia imetangaza.

Al Hilal, ilitoa tangazo hilo katika video kwenye mtandao wa kijamii, huku Neymar akisema, "Najua una wasiwasi. Mimi pia. Tarehe 21 Oktoba, narejea."

Al Hilal itamenyana na Al-Ain ya Umoja wa Falme za Kiarabu siku ya Jumatatu.

Kampuni yake ya uuzaji ya NR Sports, ilisema katika taarifa yake Jumamosi, kwamba mapenzi ya Mbrazil huyo kwa soka na matumaini yake ya kucheza Kombe lijalo la Dunia yanamrudisha uwanjani.

"Ingawa hakuna uamuzi wa mwisho wa kurejea kwake, namba 10 huyo ataweza kucheza (leo Jumatatu), ili kuendeleza maisha yake ya ajabu," ilisema taarifa hiyo.

Neymar alisajiliwa na timu ya Riyadh mnamo Agosti 2023 na alicheza michezo mitano pekee alipofanyiwa upasuaji, baada ya kupasuka mfupa wa goti lake la kushoto alipokuwa kwenye majukumu ya kimataifa Oktoba mwaka jana.

Chapisho la mtandao wa kijamii pia lililochapishwa Jumamosi, lilionesha mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 32 akizungumza kuhusu kupona kwake na alionesha picha za juhudi zake za kurejea.

"Kila wakati ninapojeruhiwa, narudi. Lakini sirudi nusu," alisema Neymar kwenye video hiyo.

Neymar alirejea mazoezini Julai, lakini Septemba kocha wa klabu yake Jorge Jesus, alizima matarajio ya kurejea mara moja. Kocha huyo raia wa Ureno hakuthibitisha Neymar atacheza siku ya Jumatatu.

# Modric avunja rekodi Madrid

**MADRID,** Hispania

KOCHA wa Real Madrid, Carlo Ancelotti, amemsifu Luka Modric, kama "mchezaji wa ajabu" baada ya kiungo huyo kusherehekea kuwa mchezaji mwenye umri mkubwa zaidi katika klabu hiyo kutoa asisti katika ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya Celta Vigo, juzi.

Bao la kustaajabisha la Kylian Mbappe liliiweka Madrid mbele katika kipindi cha kwanza, kwenye Uwanja wa Balaidos Jumamosi, na Williot Swedberg akaisawazishia Celta.

Modric kisha akatokea benchi - akivunja rekodi ya Ferenc Puskas kama mchezaji mwenye umri mkubwa zaidi wa Madrid kushiriki katika mechi ya mashindano, akiwa na miaka 39 na siku 40 kabla ya kumpa asisti Vincius Junior aliyefunga bao la ushindi.

"Ni heshima na furaha kufundisha na kufanya kazi na Modric," alisema Ancelotti akiiambia Real Madrid TV.

"Pamoja na kila kitu ambacho ameweza kufikia, yeye ni mchezaji wa ajabu na mtu wa juu."

Ushindi wa Madrid dhidi ya Celta unawaweka sawa kwa pointi na Barcelona kileleni mwa jedwali la LaLiga, kabla ya mchezo wa Barca dhidi ya Sevilla jana, Jumapili.

Pia iliongeza msururu wao wa kutopoteza katika LaLiga hadi mechi 42, mchezo mmoja chini ya rekodi inayoshikiliwa na Barcelona, ambao Madrid watakutana nao kwenye Clasico wikendi ijayo.

"Modric huwa anachangia, iwe anaanza au anatokea benchi," alisema Ancelotti katika mkutano wake na waandishi wa habari. "Ana ubora mwingi ambao unatusaidia.

"Hakuna maneno mengi ya kuongeza, bado ni mzuri. Ni mtaalamu wa ajabu, anafanya kazi kwa bidii, ni mtulivu, ana tabia nzuri, Real Madrid wana bahati kuwa na mchezaji huyu."



HABARI MICHEZO

# NBC YAFURAHIA 'DERBY' YA KARIAKOO

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI mechi ya 'Kariakoo Derby' Simba na Yanga, ikipigwa katika Uwanja wa Benjamin Mkapa juzi na kusisimua mashabiki wengi kutokana na soka la uhakika lililotandazwa, Mdhamini Mkuu wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Benki ya Taifa ya Biashara (NBC), ilifanikiwa kuipamba na kuandaa matukio kadhaa kwa ajili ya wapenzi wa mchezo huo pamoja na wateja wao.

Matukio hayo yalilenga kutoa fursa kwa wadau hao kukutana pamoja, ili kuutazama na kufurahia vizuri zaidi mchezo huo ambao ulimalizika kwa Yanga kushinda bao 1-0 katika dakika ya 86 lililopatikana kwa beki wa Simba Kelvin Kijili kujifunga wakati akiwa kwenye harakati za kuokoa.

Pamoja na kuandaa chakula cha mchana kwenye hotel ya Four Points iliyopo jijini Dar es Salaam, mahusus kwa baadhi ya wateja wake wanaoshabikia timu hizo mbili, mdhamini huyo pia aliwawezesha kwenda Uwanja wa Benjamin Mkapa wakiwa kwenye msafara maalum, ili kushuhudia mechi hiyo wakiwa kwenye jukwaa la VIP.

Shughuli zote hizo ziliongozwa na maofisa waandamizi wa benki hiyo wakiongozwa na Mkurugenzi wa Fedha, Rayson Foya, ambaye pia alipata wasaa wa kukabidhi tuzo kwa Mchezaji Bora wa Mchezo (Man of the Match), Maxi Nzengeli, kutoka Klabu ya Yanga, tukio lililoshuhudiwa na maelfu ya mashabiki waliofika uwanjani hapo na wengine wengi waliokuwa wakitazama mchezo huo kupitia matangazo ya moja kwa moja ya televisheni.

Zaidi, benki hiyo iliandaa 'screen' kubwa kwenye baadhi ya maeneo ya Jiji la Dar es Salaam, ikiwamo katika mgahawa maarufu wa Hoppipola uliopo Masaki, ili kutoa fursa kwa mashabiki wengi zaidi ambao hawakupata wasaa wa kufika uwanjani waweze kushuhudia vizuri mechi hiyo kubwa zaidi nchini Tanzania na Ukanda wa Afrika Mashariki kwa ujumla.

Awali, akizungumzia hatua hiyo wakati wa hafla ya chakula cha mchana na wateja wao, Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano na Mahusiano ya Umma wa NBC, Godwin Semunyu, alisema ni mwendelezo wa maadhimisho ya mwezi wa huduma kwa wateja wa benki hiyo, sambamba na jitihada zao kama mdhamini mkuu wa ligi hiyo kuutumia mchezo pendwa wa soka kujenga mahusiano na wateja wao sambamba na kuchochea mapenzi ya wadau hao kwa klabu zao na mchezo huo kwa ujumla.

"Udhamini wetu kwenye mchezo huu pendwa zaidi nchini na duniani kwa ujumla, umekuwa hauishii tu kulenga katika kuboresha ligi hizi tatu tunazozidhamini, bali pia tumekuwa tukihakikisha wadau wetu wote muhimu wakiwamo wafanyakazi, uongozi wa benki na wateja wetu wanakuwa sehemu ya mchezo huu kwa kushiriki moja kwa moja kwenye matukio mbalimbali, ikiwamo kushuhudia mechi kubwa kama hizi," alisema Semunyu.

Alisema benki hiyo inaendelea kubuni mikakati mikubwa zaidi ya kuiboresha ligi hiyo, ili kufikia malengo ya udhamini wake ambayo ni pamoja na kukuza vipaji na viwango vya soka nchini, kuchochea ajira kupitia michezo, kuongeza ushindani baina klabu zinazoshiriki na kuongeza hamasa ya mchezo huo nchini.

"Kila mtu ni shuhuda wa mapinduzi makubwa ambayo tayari benki ya NBC tumeyafanya katika misimu hii mitatu iliyopita ya udhamini wetu kwenye Ligi Kuu ya NBC na mwaka mmoja wa udhamini wetu kwenye Ligi ya Championship na Ligi ya Vijana," alisema.

Mbali na kuchochea ushindani kwenye ligi hizo kupitia udhamini ulioziwezesha klabu shiriki kufanya usajili mzuri, imeshuhudiwa mdhamini huyo pia akitoa huduma muhimu za kibenki kwa timu hizo, ikiwamo bima za afya, mikopo ya usafiri kwa timu na kushiriki katika kudhamini hafla mbalimbali za mchezo huo, zikiwamo zile za kukabidhi vikombe vya ubingwa pamoja na kudhamini tuzo mbalimbali za mchezo huo.




Mkurugenzi wa Fedha wa Benki ya NBC, Rayson Foya (kulia), akikabidhi Tuzo ya Mchezaji Bora (Man of The Match), kwa mchezaji wa Yanga, Maxi Nzengeli, aliyeibuka mchezaji bora wa mchezo dhidi ya Simba kwenye 'Kariakoo Derby' uliopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam juzi. Yanga ilishinda bao 1-0. **MPIGAPICHA WETU**

## Gamondi asifu ubora wa Simba

INATOKA UKURASA 24

wa kuboresha zaidi kikosi chetu kwa kuwa mbio za ubingwa bado zipo wazi," alisema.

Yanga ilipata bao pekee dakika nne kabla ya mchezo kumalizika likiwa la kujifunga kwa beki Kelvin Kijili katika harakati za kuokoa mpira uliopigwa na Maxi Nzengeli, baada ya kutemwa na kipa, Moussa Camara kutokana na faulo ya Clatous Chama.

Matokeo ya mchezo huo yanaifanya Yanga kufikisha pointi 15 na kwenda mpaka nafasi ya pili ya msimamo wa Ligi Kuu, chini ya Singida Black Stars yenye pointi 16.

Mabingwa hao watetezi wameweka rekodi ya kucheza michezo mitano, ikishinda yote, ikifikisha mabao tisa bila kuruhusu wavu wake kuguswa na kuendelea kutopoteza mechi.

Kipigo ilichokipata Simba ni cha kwanza kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu, ikishuka hadi nafasi ya nne ya msimamo ikisalia na pointi 13.

Timu hizo zitashuka tena kesho dimbani, Simba ikicheza dhidi ya Prisons, Uwanja wa Sokoine, Mbeya, saa 10:00 jioni, Yanga ikiwa Uwanja wa Azam Copmlex, Dar es Salaam, saa 1:00 usiku dhidi ya JKT Tanzania.

## LIGI KUU Z'BAR YAZIDI KUNOGA

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

VITA ya ubingwa wa Ligi Kuu Zanzibar imezidi kupamba moto huku kukiwa hakuna mbabe ambaye amepata ushindi kwa asilimia 100.

Timu ambazo hazijaonja machungu ya kupoteza hadi sasa ni nne tu, ambazo ni KVZ FC, Mlandege FC, Malindi SC na Chipukizi FC, lakini hazijashinda kwa asilimia 100, kwani zote kuna mechi zimebanwa mbavu kwa kulazimisha ama kulazimishwa sare.

Ligi hiyo inajumuisha timu 16 ambapo mwisho wa msimu, nne kutoka mkiani katika msimamo wa ligi hiyo, zitashuka daraja kwa kurudi Ligi Daraja la Kwanza kwa Kanda walizotoka, Unguja na Pambe.

Hadi kufukia sasa ligi hiyo ipo mzunguko wa saba, huku timu ya Inter Zanzibar FC ikiburuza mkia kwa kuwa na alama moja katika michezo saba aliyocheza.

Timu ya pili kutoka mkiani ni Tekeleza FC nayo ina alama moja ikiwa imecheza michezo sita, ikifuatiwa na New City FC ambayo ina pointi mbili katika michezo saba na ya nne kutoka chini ni Mwenge SC ambayo ina alama nne katika michezo saba.

Kwa upande wa timu nne za juu ni Mwembe Makumbi City ndio kinara wa ligi hiyo ikiwa na alama 15, nafasi ya pili ikikaliwa na KMKM SC yenye pointi 14 ikifuatiwa na Mafunzo FC wenye alama 13 sawa na Malindi inayoshika nafasi ya nne.

# Michezo

Jumatatu Oktoba 21, 2024

Nipashe




Rice alia na wachezaji Arsenal UKURASA 21



Beki wa Yanga, Ibrahim Hamad 'Bacca' akimchezea madhambi ndani ya 18, Kiungo Mshambuliaji wa Simba, Kibu Denis, kwenye mechi ya 'Derby ya Kariakoo' ya Ligi Kuu Bara iliyopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam juzi na Yanga kushinda bao 1-0. Hilo ni moja kati ya matukio mawili aliyochezewa Kibu, ambayo Mwamuzi Ramadhani Kayoko, analalamikiwa kwa kutotoa penalti kwa Simba. **MPIGAPICHA WETU**

## Yafahamu yaliyojiri 'Dabi' Simba, Yanga

**Na Adam Fungamwango**

MECHI ya watani wa jadi, Simba na Yanga ilimalizika Jumamosi iliyopita kwa Yanga kupata ushindi wa bao 1-0, ambapo beki wa kulia wa 'Wekundu wa Msimbazi', Kelvin Kijili, alijifunga mwenyewe katika harakati za kutaka kuokoa.

Ilikuwa ni mechi ya raundi ya nane ya Ligi Kuu Tanzania Bara, mzunguko wa kwanza iliyochezwa...



UKURASA 14

## Modric avunja rekodi Madrid

**MADRID,** Hispania

KOCHA wa Real Madrid, Carlo Ancelotti amemsifu Luka Modric kama "mchezaji wa ajabu" baada ya kiungo huyo kusherehekea kuwa mchezaji mwenye umri mkubwa zaidi katika klabu hiyo kutoa asisti katika ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya Celta Vigo, juzi.



UKURASA 22

## Hizi ndizo rekodi za Tuchel, kocha wa sasa England

**LONDON,** England

THOMAS Tuchel ameteuliwa kuwa kocha mpya wa England akichukua mikoba ya Gareth Southgate.

Tuchel amekuwa kocha wa tatu wa kigeni kuinoa England na...



UKURASA 11

# Gamondi asifu ubora wa Simba

### Afichua pia mbinu ya kuifunga, Fadlu yeye alia kunyimwa penalti huku akisema Yanga...

**Na Adam Fungamwango**

HUKU akisifu ubora wa watani wao wa jadi katika mechi ya 'Derby ya Kariakoo' juzi, Kocha Mkuu wa Yanga, Miguel Gamondi, amefichua mbinu ambayo huwa anaitumia dhidi ya Simba kuwa ni kuwashambulia pembeni hasa dakika 30 za mwisho, kwani mabeki wake mara nyingi huwa wanakuwa wameshachoka.

Akizungumza baada ya mechi ya watani wa jadi iliyochezwa juzi, Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam na Yanga kushinda bao 1-0, Gamondi alisema hata mpango wake wa kuwaingiza Clement Mzize na Kennedy Musonda, kipindi cha pili ulikuwa ni mkakati wa kwenda kushambulia kupitia pembeni kwani alijua tayari, Shomari Kapombe, beki wa kulia na Mohamed Hussein 'Tshabalala' wanakuwa wameshakuwa hoi kwa kuchoka."Kipindi cha pili niliwaingiza Mzize na Musonda, ili wakimbie kwenye nafasi za wazi, tunafahamu Simba wanashambulia sana kupitia mabeki wao wa pembeni na dakika 30 za mwisho huwa wanachoka na kuacha nafasi kila mechi. Huo ndio ulikuwa mpango wetu.

"Tulifahamu kama ilivyo kawaida, watashambulia sana dakika 15 mpaka 20 za mwanzo kisha sisi mpango wetu ni kipindi cha pili kucheza mchezo wetu tunaoufahamu na ulilipa ila nawapongeza Simba wana timu nzuri imeimarika kimbinu na hili ndio jambo zuri zaidi kupata mechi nzuri," alisema raia huyo wa Argentina.

Alimalizia kumpongea Kocha Fadlu kwa kuibadilisha Simba na kuonekana kuwa timu tishio, inayocheza kimkakati na maarifa na kwamba hilo ni jambo bora kwa soka la Tanzania.

Wakati Gamondi akisema hayo, Kocha Mkuu wa Simba, Fadlu Davids, amelia na mwamuzi Ramadhani Kayoko kwa kuwanyima walau penalti moja katika matukio mawili ya wazi kwenye mchezo huo, kutokana na mabeki wa Yanga kuonekana kumfanyia madhambi Kibu Denis, wanavyotaka huku akionekana kulikalia kimya jambo hilo.

**Fadlu alipinga kuwa Yanga ni bora kuliko wao, bali akasema wana uzoefu tu, hivyo anachoona ni kwenda kukiimarisha zaidi kikosi chake.**

Kocha huyo mbali na kumtupia lawama mwamuzi akidai timu yake imenyimwa penalti za wazi, aliisifu timu yake kuwa inazidi kuimarika kupata muunganiko na uzoefu, akidai hicho tu ndicho wanachozidiwa na Yanga.

"Si kwamba Yanga ni bora kuliko sisi, bali wana uzoefu tu, tunapaswa kuimarisha kikosi chetu na tunafahamu dirisha dogo lipo jirani, hivyo tutapas-

INAENDELEA UKURASA 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >